SportPesa
TZS. 804,667,160
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Mafuriko** abiria mikoa kaskazini yaibua gumzo

UKURASA 2



SAHA AMTABIRIA MAKUBWA MBAPPE

UKURASA 21


# Nipashe

Ijumaa Desemba 24, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579804

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper


# Mbarawa azuru bandarini usiku

●●● **Ashuhudia** msongamano wa malori, aziweka mtegoni taasisi husika... *Endelea ukurasa 2*



Baadhi ya wananchi wakinawa mikono ili kujikinga na UVIKO-19 wakati wa kuingia katika Hospitali ya Wilaya ya Ubungo ya Palestina, Sinza mkoani Dar es Salaam jana, kupata huduma. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**JELA MIAKA 20 KWA KUSAFIRISHA BANGI**

RAIA wa Kenya, Carlos Otieno (43). Amehukumiwa kifungo cha...

**NEMC: Maji ya mgodini yamejaa sumu**

UKURASA 7



Sehemu ya malori yakiwa kwenye foleni kuingia katika Bandari ya Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

# Mbaroni tuhuma za kuua kwa malipo ya 100,000/-

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA, KMC FC HAPATOSHI BARA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# ‘Mafuriko’ abiria mikoa kaskazini

**Na Waandishi Wetu**

NI mafuriko! Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na idadi kubwa ya abiria kutoka Arusha kwenda Moshi iliyoshuhudiwa jana kwenye stendi kuu mabasi jijini Arusha, wakiangaika kupa usafiri.

Baadhi ya abiria hao walionekana dhahiri kuchoka na wengine kufikia hatua ya kuketi chini kusubiri usafiri.

Nipashe ilishuhudia kwenye stendi hiyo kukiwa na abiria wengi waliobeba mabegi na wengine watoto, wakihaha kutafuta mabasi.

Gazeti hili pia lilibaini kuwa baadhi ya abiria walilazimika kuwapa fedha madalali ili kurahisisha upatikanaji wa magari kuwafikisha makwao.

John Shayo, mmoja wa abiria waliokutwa na Nipashe kwenye stendi hiyo, alidai kuwa alifika mahali huko majira ya saa tatu asubuhi lakini hadi mchana alikuwa hajapata usafiri.

“Yaani kwa kweli imekuwa shida, tena wanakuja baadhi ya vijana wanaomba niwape Sh. 1,000 ili wanipe nafasi kwenye gari linalokwenda Moshi,” alisema.

Shayo aliongeza: “Siyo hivyo tu, hata nauli ya kwenda Moshi imepanda, baadhi ya magari ya kwenda Rombo wanalazimishwa kulipa Sh.10,000 hadi 12,000 tofauti na awali kabla ya mafuriko haya ilikuwa Sh. 6,000.

Augenia Temba, alisema hali ya usafiri ni ngumu, akieleza wasiwasi wake kwamba leo itakuwa ngumu zaidi kutokana na wingi wa abiria wanaojitokeza kwenye stendi hiyo.

“Wingi wa abiria unasababisha tupandishiwe nauli kama kwenda Moshi unaambiwa lipa Sh. 5,000 au zaidi, badala ya Sh. 3,000. Kwenda Rombo Sh. 10,000 badala ya Sh. 6,000, kweli hali siyo,” alilalamika.

Aliomba serikali iwanusuru na hali hiyo kwa kuwatafutia usafiri wa dharura kwa kuwa abiria ni wengi na kuna hatari ya baadhi yao kula sikukuu stendi.

Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), Amani Mwakalebela, alipotafutwa na Nipashe kwa simu kuzungumzia suala hilo, alidai ni mgonjwa na amemtuma msaidizi wake kufuatilia kinachojiri kwa ajili ya hatua zaidi.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akipatiwa taarifa ya meli zilizoingia Bandari ya Dar es Salaam kutoka kwa Meneja wa bandari hiyo, Juma Kijavala, wakati alipotinga usiku na kukagua utendaji kazi wa bandari hiyo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbarawa azuru bandarini usiku

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amefanya ziara ya kushtukiza usiku katika Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na kutoa maagizo kadhaa kwa Mamlaka ya Mapato (TRA), Kitengo cha Huduma za Makasha (TICTS), ikiwamo kuongeza idadi ya watu katika usimamizi wa shughuli za upakiaji na upakuaji wa mizigo.

Akiwa bandarini huko Prof. Mbarawa alibaini kuwapo tatizo la msongamano wa malori wakati wa kuingia na kutoka, hivyo kuwataka wajipange kutatua kadhia hiyo.

Prof. Mbarawa pia alisisitiza umuhimu wa mawasiliano ya mara kwa mara katika taasisi hizo, ili kupunguza kero zinazowakabili na kuongeza ufanisi wa bandari.

Alisema: “Msongamano upo lakini unaweza ukatatuliwa vizuri kama kila mmoja akijipanga vizuri katika eneo lake na kuhakikisha kazi zinakwenda vizuri, mtambue fika kuwa bandarini siyo sehemu ya kumpumzika.”

Vilevile, Prof. Mbarawa aliutaka uongozi wa TPA kuwachukulia hatua mawakala wanaochelewesha vibali bandarini ikiwamo kuwafutia leseni zao.

Prof. Mbarawa pia alisema serikali imeshachukua hatua za mwanzo za kupunguza msongamano bandarini ikiwamo kuyaruhusu malori yote yanayobeba mafuta kupita bila ya kupima, kwamba kuna vituo maalumu ambavyo vimewekwa kwa ajili ya malori hayo.

Prof. Mbarawa alikerwa na tabia ya mawakala wa mizigo kutokukamilisha taratibu zote za vibali kwa wakati na hivyo kusababisha malori kukaa bandarini hapo wakisubiria kwa muda mrefu.

“Kuanzia sasa lazima magari yanayoingia bandarini yawe na vibali vya kutosha, hapa siyo mahali pa kukaa na kulala siku tatu au nne, hakikisheni mnawachukulia hatua kali mawakala wote hata kama ni kufutiwa leseni zao katika ucheleweshaji wa vibali kwani wao ni tatizo kubwa bandarini hapa,” aliagiza.

Hata hivyo, waziri huyo alipongeza uongozi wa TPA kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kuwa mzigo ni mwingi na meli zilizoko nje zinasubiria kuingia ni nyingi na kuwataka kuendelea kufanya kazi usiku na mchana kuhakikisha hakuna kinachoharibika na kuendelea kuingizia mapato nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Eric Hamiss, alisema wamepata baraka ya kupata mizigo mikubwa katika Bandari ya Dar es Salaam, akibainisha kuwa nje kuna meli 18 zinasubiria kuingia na ndani meli 13 zinaendelea kushusha mzigo.

Aliishukuru serikali kwa kuruhusu malori yanayobeba mafuta kutopima katika mizani bandarini huko na kwa hali ya sasa foleni imepungua kwa kiasi kikubwa.

Kuhusu suala la malori yasiyo na vibali, Erick alieleza kuwa kuanzia Januari mosi mwakani hakutakuruhusiwa malori kuingia bandarini kama wakala hajakamilisha taratibu zote za vibali.

# Matatani madai ya kuua kwa malipo ya 100,000/-

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MTU mmoja anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za mauaji baada ya kuahidiwa Sh. 100,000 kutekeleza mauaji hayo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na mwili wa marehemu uligundulika Desemba 11, mwaka huu.

“Katika hali isiyo ya kawaida, aliahidiwa kupewa shilingi laki moja na alitanguliziwa Sh. 40,000 ili kutekeleza mauaji hayo,” alisema Kamanda Issah.

Alisema siku ambayo polisi walikwenda kuangalia tukio, waliukuta mwili wa marehemu na pikipiki aliyokuwa nayo ilichukuliwa na mtuhumiwa na kutamba nayo mjini.

“Muuaji alichukua pikipiki ya marehemu na kutembea tembea nayo mjini na alipokamatwa nayo na kuulizwa, alidai amepewa kazi ya kuua na kupewa Sh. 40,000 huku akiwa anadai Sh. 60,000 kukamilisha ahadi aliyopewa,” alisema Kamanda.

Kamanda alisema baada ya taarifa hizo, walimsaka mtu aliyetoa pesa hizo na kumtia mbaroni.

“Eti tuna muhoji kwanini mmemuua anasema walikua wanagombea mashamba, na kama mnagombea mashamba sheria zipo. Tunashauri Wananjombe fuateni sheria, acheni kujichukulia sheria mikononi,” alionya.

Wakati huo huo, jeshi hilo limesema limejipanga kuhakikisha usalama wa maeneo yake kipindi cha Sikukuu za Krismas na Mwaka Mpya.

“Tumejipanga vizuri kuanzia sehemu za ibada, makazi ya watu mpaka maeneo ambayo watu wanasherehekea na kutokana na hali kama hiyo, tumejipanga pia kufanya doria za miguu, magari, pikipiki na doria fiche ambazo zitakua zinaangalia maeneo yenye uhalifu sugu,” alisema.

Pia alisema jeshi la polisi litashirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kuhakikisha usalama wa Njombe unakuwapo na kuendelea kuwa na utulivu kwa muda wote wa sherehe ambazo zinaendelea.

Aliwataka wananchi kuepuka misongamano isiyo ya lazima ili kuepuka ugonjwa wa Uviko-19.

HABARI KITAIFA

# Waziri mbogo urasimu TBS

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, ameshangazwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuwakwamisha baadhi ya wawekezaji wa viwanda vya dawa licha ya taasisi zingine kuwapatia vibali kwa wakati.

Waziri Mkumbo aliyasema hayo jana alipofanya ziara kukagua viwanda katika eneo la Kibaha baada ya kiwanda cha kuzalisha chanjo za wanyama na ndege cha Hester Biosciences Africa Limited kulalamikia kukwamishwa kibali na TBS na bidhaa zake kukwama uwanja wa ndege.

Awali Mratibu Mkuu wa kiwanda hicho, Tina Sokoine, alisema bidhaa zao zimekwamishwa na TBS licha ya taasisi zingine kuwapatia zikiwamo Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Mamlaka ya Mapato Tazania (TRA), TASAC jambo ambalo linaweza kuwasababishia hasara kubwa.

Alisema bidhaa hizo ambazo zitatumika kutengeneza chanjo huziagiza nje ya nchi na zinatakiwa kuwekwa kuwa kwenye ubaridi ambao unatakiwa, hivyo TBS inavyowachelesha katika kutoa mzigo wanawafanya wafanye kazi katika mazingira magumu.

"Hii kukwamisha na kusababisha uharibifu na hasara kwa mizigo ambayo inahitaji uangalizi maalum hasa yenye mnyororo wa ubaridi na tunatumia gharama kubwa kuagiza hizi bidhaa mpaka sasa TBS ndio wametuchelewesha na mzigo umebidi ulale airport (uwanja wa ndege)," alisema.

Baada ya kusikiliza maelezo hayo Waziri Mkumbo alisema kuna changamoto ya mwingiliano wa taasisi katika kuwahudumia wawekezaji ni vyema suala linalohusu dawa likashughulikiwa na TMDA badala ya TBS kuwakwamisha.

"Kwa mfano TBS na TMDA tutakwenda kuliangalia hili. Mwelekeo wa serikali ni kwamba taasisi moja iweze kufanya majukumu mengi iwezekanavyo kwenye haya mambo ya viwanda vya dawa pamoja na chanjo hatuoni kwa nini TBS iingie sana kwa sababu TMDA ipo.

"Tunaenda kuliangalia ndani ya serikali lengo la serikali ni kuhakikisha kwamba tunawarahisishia wawekezaji mazingira ili waweze kufanya kazi kwa urahisi zaidi."

Pia Mkumbo alisema mtaa huo wa viwanda ambao upo Kibaha ni eneo kubwa lenye zaidi ya heka 200 wana viwanda vikubwa vitatu ikiwamo kiwanda cha dawa cha chanjo ya wanyama, viwanda vya kuunganisha magari, kiwanda cha kutengeneza vifungashio mbalimbali.



Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, akitoa maelekezo kwa maofisa madini katika soko la madini Kahama, juu ya utoaji wa namba za malipo kwa wafanyabiashara wakati wa uuzwaji wa madini, alipofanya ziara ya kushtukiza sokoni hapo jana, kulia kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Jela miaka 20 kusafirisha bangi magunia 89

**Na Samson Chacha,** TARIME

RAIA wa Kenya, Carlos Otieno (43). Amehukumiwa kifungo cha miaka 2o jela baada ya kupatikana akisafirisha magunia 89 ya bangi yenye uzito wa kilogramu 2,830.2 ya dawa za kulevya aina ya bangi.

Otieno mkazi wa kaunti ya Migori mkoa wa Nyanza, alikamatwa akisafirisha mihadarati hiyo kwenye lori lenye namba za usajili KAS 924 U alilokuwa akiliendesha kutoka kijiji cha Kitagasembe wilayani Tarime kwenda kuuza nchini Kenya.

Licha ya kuhukumiwa jela kutumikia kifungo hicho, lori lililokutwa na dawa hizo za kulevya limetaifishwa kuwa mali ya serikali.

Akisomewa hukumu hiyo juzi, Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Musoma, Frank Mahimbali katika kikao cha mahakama kinachoendelea wilayani hapa, akishirikiana na wazee watatu wa mahakama, alisema ameridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka bila kuacha chembe yoyote ya shaka.

Awali, Mwanasheria wa Serikali, Mafuru Moses, alidai kuwa mtuhumiwa mnamo Mei 26, 2016 alfajiri saa 12:00, alikamatwa na polisi wa Kituo cha Sirari waliokuwa doria katika kijiji cha Kitagasembe akiwa dereva wa lori aina ya Mitsubishi Fuso.

Moses alidai kuwa askari hao walipomkamata, walimhoji anatoka wapi na amebeba nini, hivyo kushindwa kuwajibu kutokana na kuwa na hofu ndipo walipomtilia shaka na mzigo uliobebwa ndani ya lori hilo na kumuamuru kuendesha hadi kituo cha polisi Sirari huku wakiongozana naye.

"Lori lilipofika kituoni, Polisi waliita mashuhuda wakiwamo ofisa mtendaji wa kata ya Sirari na maafisa wengine wa vijiji wakati wanalifungua.

"Walipofungua lori hilo walikuta magunia 89 ya bangi iliyokauka yenye uzito wa kilo 2,830.2 iliyokuwa imefungwa kwa umakini, hivyo kumweka mtuhumiwa chini ya ulinzi," alidai.

Katika kesi hiyo, upande wa mashtaka ulipeleka mashahidi saba wakiwamo wakemia wa maabara ya dawa za kulevya pamoja na vielelezo saba.

Mshtakiwa hakuwa na shahidi bali alijitetea na kudai kuwa yeye si dereva na hajui kuendesha gari. Alidai kuwa wakati anakamatwa, alitoka kwake Migori nchini Kenya na kusafiri kwenda Sirari upande wa Tanzania kununua mchele kwa ajili ya matumizi lakini alipofika Sirari mpakani alikamatwa na kufikishwa kituo cha Sirari na kufunguliwa kesi ya kusafirisha bangi.

Otieno aliiomba mahakama kumwonea huruma kwa madai kuwa amekaa gerezani tangu 2016 hadi sasa na kwamba ana mke na watoto wawili wanaosoma.

Baada ya utetezi huo, Jaji Mahimbali alisema kutokana na ushahidi uliotolewa kwa upande wa mashtaka kupitia mashahidi saba na vielelezo tisa, anamhukumu Otieno kifungo cha miaka 20 jela.

Hata hivyo, Jaji alisema kutokana na muda wa miaka sita aliokaa gerezani, mshtakiwa atatumikia kifungo cha miaka 14 jela na kwamba nafasi ya kukata rufani iko wazi.

Mtuhumiwa alishtakiwa kwa Kifungu cha 15 (1)b cha Sheria Na. 5 ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya ya mwaka 2015 juu ya makosa ya kusafirisha, kuuza na kupatikana na dawa za kulevya.

Aidha, kwa mujibu wa Sheria ya Makosa ya Jinai (CPA) kifungu cha 49 (1), chombo kinachopatikana kimebeba au kusafirisha mali isiyo halali ikiwamo biashara za magendo na dawa za kulevya, hutaifishwa na kuwa mali ya serikali.

"Pia madhara yanayotokana na dawa za kulevya ni pamoja na utegemezi, ugomvi, kuharibu mfumo wa akili ya binadamu kwa watumiaji," alidai Mafuru.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA**
**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU**
**WILAYA YA GEITA**
**SHAURI LAMADAI NAMBARI 63/2021**

**MDAI: AMINA RAJABU ABDALAH**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: MAGEMBE MOSES**
**WA**

**POPOTE ALIPO BARA NA VISIWANI**
**AMRI:**

Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 27/12/2021 Saa 2:30 Asubuhi bila kukosa.
Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo,na kutolewa uamuzi.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo Jumatano tarehe 08 mwezi 11/ 2021

..........................................................
**HAKIMU**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**FATIMAH AUNALI MOHAMMEDALI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0437/0011** kilichotolewa Baraza na Mitihani la Taifa kupitia **ALMUNTAZIL SEKONDARI** mwaka **1994.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/GOG/RB/599750/2021.**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**RAYMOND REGINALD MARIKI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 310 BKH – SUZUKI GRAND VITARA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/79913/2021.**

RIPOTI MAALUMU -2

# Simulizi mwanafunzi aliyebakwa na mchunga ng'ombe kichakani

## ■Bodaboda wajiwekea masharti

Na Elizabeth Zaya, aliyekuwa MPWAPWA

UFUNGUZI wa ripoti hii jana uliwasilisha haiba ya maisha ya binti mwanafunzi anavyokutana na madhila, ikiwamo safari ya muda mrefu kwenda na kutoka masomoni, hata kuishia kunusurika kuwa kitoweo cha mnyama na tukio la kubakwa lililomhamisha kutoka kwenye uanafunzi hadi uzazi.

Endelea na sehemu nyingine kufuatilia misukosuko inayompata binti huyo, ambayo inaakisi mengi yanayowapata wenye jinsia ya kike, umri na maisha kama ya kwake anakoishi:

Sarah Chakutemana, mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Ving'hawe iliyoko Mpwapwa, anasema alifaulu na kupata nafasi ya kujiunga na Shule ya Sekondari Mazai iliyoko nje kidogo ya Mji wa Mpwapwa lakini alilazimika kuhama akiwa kidato cha kwanza kutokana na umbali mrefu aliokuwa anatembea kwenda shuleni na kurudi nyumbani.

Anasimulia kuwa wakati anaanza masomo kidato cha kwanza, alibaini kwamba wanafunzi waliokuwa wakitokea mjini Mpwapwa kwenda kusoma katika shule hiyo hawakuwa wengi, hivyo kujikuta kila siku akitembea barabarani peke yake kwenda na kurudi.

"Ili kufika shuleni, nilikuwa ninapita kwenye njia za vichakani mwanzo-mwisho, huko unakutana na wachunga mifugo na wanaokwenda mashambani, ni mwendo wa saa moja na nusu mpaka kufika lakini cha moto nilikuwa ninakiona.

"Mwezi mmoja tu wa kidato cha kwanza nilikuwa sitamani tena shule, maana nilikuwa nachelewa kila siku na ninachapwa viboko au kupewa adhabu na nikawa nakosa baadhi ya vipindi.

"Nilimwambia baba yangu kwamba wasiponihamisha, naacha shule. Nilinusurika kubakwa mara nyingi sana na wale wachunga ng'ombe porini, ilikuwa haipiti hata siku moja hawajakusimamisha njiani kukutongoza.

"Mbinu niliyoitumia ili wasinibake ni 'kutowakazia sana', akinitongoza ninakubali, lakini 'ninampiga saundi' (kutoa ahadi za uongo) ili kujenga urafiki nao," anasema.

Hata hivyo, Sarah anabainisha kuwa mbinu yake hiyo haikuchukua muda mrefu kushtukiwa, akieleza kuwa hawakuacha kumtaka kimapenzi na hata kutishia kumbaka.

"Mara nyingi nilipokutana na hatari ya kubakwa nililazimika kukimbia na kupiga kelele kuomba msaada kwa wapita njia, hivyo wachunga ng'ombe wanaogopa kuendelea na dhamira yao hiyo.

"Nakumbuka siku moja wakati natoka shuleni jioni, nikakutana na mmoja alikuwa anaswaga ng`ombe kuwarudisha nyumbani, akasema tukae tupige stori, nikamwambia 'hapana giza linaingia tutafanya hivyo kesho', nikaendelea na safari.

"Akaacha mifugo yake, akanifuata. Nilitimua mbio ambazo sikuwahi kukimbia na bahati nzuri kulikuwa na watu mbele, ninafikiri walikuwa wanatoka shambani, ndipo akarudi.

"Siku hiyo ndipo nilisema 'sasa basi, naona elimu siyo ridhiki yangu!' Niliporudi nyumbani nikamwambia baba 'kama hataki kunihamisha, siendi tena shuleni' na ikabidi nimwambie ninayokutana nayo huko njiani. Nilikaa nyumbani mpaka aliponitafutia uhamisho," Sarah anahitimisha.



Mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Matomondo akivuka Mto Mamba wilayani Mpwapwa mwanzoni mwa mwezi huu. PICHA: ELIZABETH ZAYA

> "Akaacha mifugo yake, akanifuata. Nilitimua mbio ambazo sikuwahi kukimbia"

### USHUHUDA BODABODA

Simioni Luhembe, dereva wa pikipiki ya kubeba abiria, maarufu bodaboda, anasema awali walikuwa wanasaidia kuwabeba wanafunzi angalau wawili au watatu kwa kila pikipiki walipowakuta njiani lakini waliacha kufanya hivyo mwaka jana baada ya baadhi yao kukamatwa na kuwekwa mahabusu, wakituhumiwa kuwapa ujauzito baadhi ya wanafunzi.

"Kwa sasa hatudhubutu hata kidogo kuwasaidia kuwabeba wanafunzi wa kike kwa sababu mwaka jana yalitokea majanga makubwa sana, wanafunzi wengi kutoka katika shule hiyo walipata mimba na watuhumiwa waliosombwa wengi na kuwekwa ndani (mahabusu) walikuwa madereva bodaboda.

"Mpaka sasa baadhi yao bado kesi zao zinaunguruma mahakamani. Wanafunzi wa kike tunawaogopa kama ukoma. Hata kama unaona giza lile linaingia au wingu kubwa la mvua unaliona hatuwabebi, bora tuwabebe wanafunzi wa kiume kuliko hao wa kike.

"Hata maji yakijaa hapa mtoni hatuwavushi, wanapambana wenyewe, tunawaangalia tu, mtu akishindwa arudi kwao akalale au arudi shuleni akalale darasani. Kikubwa cha kuiambia serikali ni kuwajengea hosteli ili wakae shuleni, la sivyo watakuwa wanabebeshwa mimba tu," alionya.

Dereva bodaboda huyo pia anashauri serikali iangalie namna bora ya kuwasaidia wanafunzi wote wanaosoma katika shule za msingi na sekondari zinazozunguka Mto Mamba.

Alivitaja vijiji vinavyozunguka mto huo kuwa ni Mang`weta, Mseta, Tambi, Mboli, Gengetisa na Gulwe.

Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 inaelekeza "Serikali itaweka mazingira bora na kuhakikisha kuwa sekta ya elimu na mafunzo ya ufundi inatoa rasilimali watu ya kutosha na mahiri ili kukidhi mahitaji ya sekta mbalimbali kwa maendeleo ya taifa."

### KAULI YA DED

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mpwapwa, Mwanahamisi Ally, anakiri baadhi ya wanafunzi katika halmashauri hiyo kutembea umbali mrefu kupata elimu.

Anasema mikakati iliyopo kukabiliana na kero hiyo inajumuisha ujenzi wa hosteli lakini kuna tatizo la kwenye baadhi ya shule zenye huduma hiyo, baadhi ya wazazi kuzuia watoto wao kuishi hosteli.

"Yaani mwamko wa wananchi wa huku bado upo chini sana. Kuna baadhi ya shule tumejenga hosteli, lakini wazazi wamegoma kupeleka watoto wao eti kwamba wanatumia gharama kubwa.

"Baada ya kufanya uchunguzi tulibaini kwamba baadhi yao wanatanguliza maslahi yao binafsi, wanawashawishi wanafunzi wapange kwenye nyumba zao mitaani badala ya kwenda hosteli za shuleni, hili bado tunapambana nalo.

"Na hili ni miongoni mwa shida zinazochangia baadhi ya wanafunzi kupata ujauzito, kwa sababu wanakuwa wanarubuniwa huko mitaani," anaonya.

### OFISA ELIMU

Kwa mujibu wa Ofisa Elimu Taaluma Msingi katika Halmashauri ya Mpwapwa, Agnes Mkacha, wanafunzi wa kike waliosajiliwa kufanya mtihani wa darasa la saba mwaka 2019 walikuwa 3,649 lakini waliofanya mtihani huo ni 3,553, huku 96 wakishindwa kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo utoro.

Alisema mwaka 2020, wanafunzi wa kike waliosajiliwa kufanya mtihani wa darasa la saba walikuwa 3,485. Kati yao, waliofanya mtihani walikuwa ni 3,388, huku wengine 97 wakishindwa kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo utoro.

Ofisa Elimu huyo alibainisha kuwa kwa mwaka huu, wanafunzi wa kike waliosajiliwa kufanya mtihani huo walikuwa 3,826, waliofanya ni 3689 na 137 hawajaufanya kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo utoro.

Ripoti iliyotolewa na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) mwaka jana, inabainisha kuwa tatizo la wanafunzi kukatisha masomo katika shule za sekondari lipo zaidi katika madarasa ya chini.

Inafafanuliwa kwenye ripoti hiyo kwamba kidato cha pili waliokatisha masomo mwaka huo walikuwa asilimia 39.6 na sababu zake ni utoro (asilimia 91.6) na mimba (asilimia 5.5).

HABARI KITAIFA

# Watu 61 mbaroni tuhuma za uhalifu

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam linawashikilia watu 61 kwa tuhuma za kujihusisha na makosa mbalimbali ya kihalifu ikiwamo unyang'anyi wa kutumia silaha, dawa za kulevya na uporaji.

Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi (ACP) Jumanne Muliro, alisema jana kuwa ukamataji huo ni matokeo ya operesheni maalumu ya kuzuia vitendo vya kihalifu iliyofanyika kuanzia Desemba Mosi hadi 22, mwaka huu.

Alibainisha kuwa miongoni wa watuhumiwa wanaoshikiliwa ni Yohana Zakaria, maarufu kama Cobra, na wenzake saba ambao wanadaiwa kujihushisha na vitendo vya unyang'anyi wa kutumia silaha bandia na kujipatia fedha na vitu vingine vya thamani katika maeneo mbalimbali Dar es Salaam.

"Taratibu za kisheria zinakamilishwa ili watuhumiwa hao wafikishwe mahakamani. Pia wengine saba wanashikiliwa kwa kujihusisha na wizi wa vifaa vya kielektroniki maeneo ya Mabwepande, Mbweni, Kinondoni na maeneo mengine ya Dar es Salaam na kwenda kuuzwa wilaya ya Kibiti mkoani Pwani.

"Vitu hivyo ni televisheni 22 zenye ukubwa wa aina tofauti, redio mbili, kompyuta mpakato tano na gari aina ya Subaru lenye namba za usajili T 410 DUS na uchunguzi unaendelea," alisema Muliro.

Aliongeza kuwa wamewakamata pia watuhumiwa watano wanaume wakiwa na dawa za kulevya aina ya Heroine gramu 16 na wengine 34 wa kiume 31 na wa kike watatu wakiwa na bangi kilogramu 13 na gramu 301.

Muliro alisema jeshi hilo pia limewakamata watu watatu kwa tuhuma za kuvunja maghala ya wafanyabiashara kwa kutumia funguo bandia na kuiba vitu ikiwa ni pamoja na vitabu vya kumbukumbu 49, fedha za sarafu zenye thamani zaidi ya Sh. milioni 1.6, viyoyozi na balbu sita.

"Pia watuhumiwa watatu wakiume wanaojihusisha na wizi wa vifaa vya magari katika wilaya ya Ilala wamekamatwa wakiwa na side mirrors 24, reverse camera sita, alarm remote nne, honi mbili na central lock moja.

"Vifaa vingine ni nembo moja ya gari aina ya Landcruiser, twitter 7, air condition vent moja na bulbu sita za mwanga mkali. Na watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani baada ya uchunguzi kukamilika," alisema Muliro.

Pia alisema katika kuelekea sherehe za Krismasi na Mwaka Mpya, Muliro aliwataka wananchi kuhakikisha mtu mmoja au zaidi wanabaki nyumbani wakati wa kwenda matembezini au kwenye ibada.

Alisisitiza wazazi na walezi kutowaacha watoto kwenda matembezi bila uangalizi maalumu, mtu kuepuka kuendesha gari akiwa ametumia kilevi huku akidai kuwa madereva watakaotiliwa mashaka watapimwa na watakaobainika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Pia aliwataka madereva wa vyombo vya moto na watumiaji wengine wa barabara kuzingatia sheria na taratibu za usalama barabarani ili kuepusha ajali zisizokuwa na ulazima, pamoja na kujiepusha na uchomaji wa matairi au uharibifu wa miundombinu kwa kigezo cha kusherehekea.

Alipiga marufuku kufanya milipuko ya aina yoyote baruti au fataki pasipokuwa na kibali, pamoja na kutoa taarifa za wahalifu na uhalifu uliopo katika maeneo yanayowazunguka katika kituo chochote cha polisi au kwa kupiga 111 au 112.

"Jeshi la Polisi kanda maalumu limejiimarisha vyema katika kuhakikisha mifumo ya kuzuia vitendo vya kihalifu inasimamiwa vizuri ikiwa ni pamoja na doria na misako ili wananchi washerehekee kwa amani na utulivu siku kuu za Krismas na Mwaka mpya.

"Hivyo natoa tahadhari na onyo kali kwa mtu au kikundi cha watu chenye lengo la kufanya vitendo vya kihalifu kutojihusisha na matendo hayo maovu," alisisitiza Muliro.



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira Dk. Samuel Gwamaka akiwa na watalaamu wa NEMC pamoja na wataalamu wa kutoka maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wakikagua taka hatarishi iliyotupwa eneo la Visegese, Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kibano chanukia waliofunga ving'ora, vimulimuli magari binafsi bila kibali

**Na Rose Jacob,** MWANZA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhan Ng'anzi, amewataka wakuu wa taasisi, ofisi na watu binafsi waliofunga ving'ora na vimulimuli kwenye magari kinyume cha sheria kuviondoa haraka.

Akizungumza jana ofisini kwake, Kamanda Ng'anzi, alisema kumezuka tabia ya baadhi ya wamiliki na madereva kushindwa kufuata sheria za usalama barabarani ambazo zinatambua baadhi ya magari yanayofungwa ving'ora na vimulimuli.

"Magari yote yaliyofungwa ving'ora na vimulimuli ambayo hayahusiki katika dharura kuanzia sasa yatakamatwa na kung'olewa vifaa hivyo na wahusika watakamatwa na kushtakiwa," alisema.

Pia kamanda huyo alisema madereva wote ambao leseni zao hazikidhi viwango au zimeisha muda, wafuate kanuni la sivyo watakamatwa na kufunguliwa mashtaka.

Naye Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Wilbroad Mutafungwa, alisema kwa yoyote atakayeshindwa kufuata sheria za usalama barabarani hasa katika kipindi cha sikukuu za mwisho wa mwaka kwa kufanya makosa hatarishi barabarani yanayoweza kusababisha ajali na vifo, atachukuliwa hatua.

'"Hatutakuwa na huruma kwa mtu yeyote atakayetenda makosa haya hususani ulevi, mwendo kasi, kutoheshimu vivuko vya waenda kwa miguu, kuyapita magari mengine bila kuchukua tahadhari, kupakia mishikaki, kutovaa kofia ngumu, kutofunga mkanda, kuzidisha abiria, ubovu wa magari na abiria kupakiwa kwenye magari ya mizigo," alisema Mutafungwa.

Kamanda Mutafungwa alisema takwimu za oparesheni walizofanya kuanzia Desemba Mosi hadi 20, mwaka huu zinaonyesha kuwa magari yaliyokaguliwa ni 122,950 na yaliyopatikana na ubovu ni 17,886 na magari yanayosafirishwa nje ya nchi (IT) yaliyokamatwa ni 1,024.

## Madereva walevi sikukuu lupango

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, limewaonya madereva wa vyombo vya moto, ambao wanaendesha wakiwa wametumia vilevi na kusababisha ajali, kuwa watakula sikukuu za mwisho wa mwaka wakiwa mahabusu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, George Kyando, alisema jana kuwa madereva ambao watakamatwa wametumia vilevi hivyo, watapelekwa mahabusu katika Gereza la Wilaya ya Shinyanga, Mhumbu, hadi hapo sikukuu zitakapokwisha ndipo watatolewa.

Kyando alisema jeshi hilo limejipanga vyema kuimarisha ulinzi na usalama kwa wananchi na kuzuia ajali katika sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya.

Alisema katika msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka, huwa kuna ongezeko la ajali za barabarani, ambazo baadhi husababishwa na madereva wazembe kwa sababu ya kutumia vilevi na kuonya kwamba jeshi hilo litawakamata na kuwasweka mahabusu.

"Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, tumejipanga vyema kudhibiti ongezeko la ajali za barabarani kwa kufanya ukaguzi wa kupima vilevi, madereva wote wa vyombo vya moto na tutakaowakamata tutawapeleka mahabusu hadi sikukuu zipite," alisema Kyando.

"Kwenye vyombo vya habari mmesikia kuwa gereza la Wilaya ya Shinyanga limejaa wafungwa na mahabusu, hiyo ndiyo kazi ya Jeshi la Polisi. Tutawakata madereva wote walevi na kuwapeleka huko," aliongeza.

Aidha, Kyando alisema jeshi hilo limejipanga kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo yote ya ibada na kuonya watu ambao wamepanga kufanya uhalifu katika sikukuu hizo waache mara moja.

Katika hatua nyingine, jeshi hilo limepiga marufuku disko toto, upigaji wa baruti na uchomaji wa matairi hasa wakati wa kusheherekea Mwaka Mpya.

Baadhi ya wananchi wa Shinyanga, walitoa wito kwa jeshi hilo kufanya kazi zao kwa vitendo, kudhibiti uhalifu na ajali katika msimu huu wa sikukuu za mwisho wa mwaka badala ya kuzungumza kwenye vyombo vya habari.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tusifanye mchezo UVIKO-19 ipo, tukachanje

**JANA** Wizara ya Afya, imetangaza kuwapo kwa maambukizi ya UVIKO-19 na kuwataka Watanzania kuchukua tahadhari kwa kujikinga ipasavyo kwa kuvaa barakoa, kuepuka misongamano na kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka na kupaka vitakasa mikono.

Pia Waziri wa Afya, Dk. Dorothy Gwajima, amesema kati ya watu wanaougua 10, vifo saba vinatokea kwa watu ambao hawajachanja na kuwataka Watanzania kuchanja ili kuwa salama kwa kuwa chanjo zipo na lengo la serikali ni kuwafikia watu zaidi ya milioni 35.

Taarifa hizi za wazi zilizotolewa na serikali za hali ya maambukizi nchini, zitaamsha wengi kuchukua hatua ya kujikinga na kwenda kuchanja.

Kwa ujumla hali sio nzuri kwa kuwa sasa serikali inadhihirisha kuwa janga hilo limerudi kwa kasi nchini, katika kipindi hiki ambacho Watanzania wengi wamekwenda vijijini na miji mingine kuungana na wanafamilia kusherehekea sikukuu za mwisho wa mwaka.

Itakumbukwa mwezi Machi, mwaka huu, mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara ilikuwa katika wakati mgumu kutokana na ongezeko kubwa la maambukizi ya UVIKO-19, katika kipindi ambacho kulikuwa na baridi.

Wataalamu wanasema kirusi hicho hupata nguvu kwenye baridi na ndiyo maana kumekuwa na kupanda na kushuka kwa maambukizi kutegemeana na hali ya hewa.

Ni muhimu sana serikali na viongozi wa dini ikahimiza watu watakaoshiriki ibada za mwisho wa mwaka au Ijumaa na Jumapili, kuhakikisha wanaingia maeneo hayo wakiwa wamevaa barakoa, kunawa mikono na kutumia vitakasa mikono.

Pia kwenye sherehe mbalimbali tahadhari ichukuliwe ipasavyo ili kuhakikisha waliokwenda vijijini hawawi sehemu ya chimbuko la kusambaza maambukizi kwenda vijijini au kwenda mjini.

Hali hii haikwepeki kuhimiza watu kuchanja hata kwa wataalamu kupata nafasi kwenye nyumba za ibada kueleza umuhimu wa chanjo na faida ya kuchanja ili kuongeza idadi ya wanaochanja.

Tunaamini ikiwa kasi ya kuelimisha umma kwa mifano halisi kutasaidia wengi kuelewa umuhimu na kuchukua hatua ya kuchanjwa kwa kuwa kila mmoja anataka kuendelea kuishi.

Lazima tuwaeleze watu mifano ya nchi za Afrika zilizofanikiwa kwenye chanjo, Ulaya na Marekani ambao sasa wanaishi bila hofu kwa kuwa wengi au wote wamepata chanjo.

Kama wao wameweza basi hata Tanzania inaweza kuingia kwenye historia ya kuchanja watu wengi na kudhibiti maambukizi ya UVIKO-19 na kila mtu kuendelea na shughuli zake kama kawaida.


Ni vyema watu wakatambua kuwa hata kama utachanja ni muhimu kuendelea kuchukua tahadhari kwa kuwa hata ukichanja unaweza kupata maambukizi, lakini haitakuwa makali kama ambaye hajachanja.

Ipo mifano hai ya ambao hawajachanja walivyopata ugonjwa huo na ambao wamechanja, kwa ambao wamechanja wameugua lakini hawakulazwa au kuwekewa mashine ya kuwasaidia kupumua na kulazwa chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu.

Ikiwa nyumba za ibada, sokoni, kwenye minada na kwingine kutatumika vyema kutoa elimu ya kujikinga na kuchanja, tunaamini Watanzania wengi watachanja na kuwa salama zaidi.

Lazima kutoa elimu sahihi ili kuondoa hisia mbaya zilizojaa kwenye vichwa vya watu kuwa chanjo sio salama na mengineyo ambayo yamerudisha nyuma utayari wa watu kuipokea na kukubali chanjo licha ya kwamba ni bure.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Upepo huu wa mafua unaoendelea, unatukumbusha chanjo ni muhimu

Na Adam Fungamwango

**UNAPOSALIMIANA** na watu hivi sasa, wanne kati ya kumi watakwambia anaumwa. Inawezekana hata anayewasalimia, pia naye ana tatizo hilo hilo.

Kwa sasa, kwenye nchi yetu na dunia nzima kumezuka na tatizo la homa kali, kifua na mafua, kichwa na viungo kunyong'onyea. Ni tatizo lilionekana kuanza kukumba wengi nchini mwanzoni mwa Novemba. Tumesikia hata wachezaji wa timu kubwa za soka nchini Simba, Yanga, Azam, Mtibwa Sugar, JKT na zingine wakipata tatizo hilo.

Mitaani ndiyo kabisa! Kumekuwa na watu wengi waliopatwa na maambukizi ya ugonjwa huo wa homa na kukohoa na mafua makali.

Ni ugonjwa ambao unasababisha kichwa kuuma, kwenye maungio kama vile kwenye magoti na katikati ya mikono kuuma kama mtu aliyepigwa.

Yupo rafiki yangu mmoja alinipigia simu na kuniambia anaumwa yeye, mkewe, watoto watatu na mfanyakazi wake wa ndani. Mama mmoja nilimuona anakwenda hospitali akiwa na watoto wake wawili wadogo, wote wakiwa wamekumbwa na tatizo hilo. Kila mtu anaonekana kushangaa ni upepo gani mbaya ambayo umepita. Wengine wakidai ni mvua za ghafla zilizonyesha na baadaye kuacha, ndizo zilizobadili hali ya hewa na watu wanaanza kuumwa.

Nakumbuka wakati chanjo za ugonjwa wa Covid -19 zilipoanza, wengi walionekana kuzipinga kwa sababu mbalimbali ambazo walikuwa wanazitoa.

Wapo waliosema kuwa huenda baadaye wakawa na matatizo ya kuzaa. Wengine wakadai kuwa zinaweza kusababisha kuua nguvu za kiume. Kuna walioenda mbali sana na kudai kuwa huenda wangegeuka 'mazombi'.

Wale wanaopenda kuangalia filamu za watu wa kutisha wanaweza kuelewa zaidi, inawezekana hawa zamani ndiyo walikuwa wanaitwa mazimwi.

Hadi leo hatujawahi kuona hata mtu mmoja tunayemfahamu aliyechanjwa amegeuka zombi.Wataalamu wakabainisha kuwa siyo kama mtu ukichanja basi huwezi kupata kabisa maambukizi, la hasha.

Ila kinachosaidia ni kwamba ukichanja, bali unakuwa na kinga hata kama ikija, basi mwili unaweza kukabiliana na misukosuko ya nguvu ya ugonjwa wenyewe. Hii imeanza kuonekana kwani wengi ambao walikuwa hawataki kuchanja, au kukimbia kwa sababu mbalimbali ndiyo wanaoonekana kupigwa sana na homa hii, kuliko ambao wameshachanjwa. Ndiyo maana unaweza kumuona mtu anaumwa, lakini bado anakwenda kazini, anafanya shughuli zake kama kawaida. Anachofanya ni kufuata maagizo tu ya wataalamu ili asiambukize wengine, kuambukizwa na kufuata matibabu mengine, ili apone haraka.

Mfululizo wa homa hizi hizi, zimewapata wengine ambao wamekimbilia hospitalini na kuwalaza, wengine wamelala majumbani hawajiwezi kutokana na kuumwa sana kichwa, kifua, kukohoa na kukosa nguvu.

Ukifuatilia kidogo, utakuta hawa ni wale ambao walikuwa wakipuuzia chanjo. Mbali na hilo, hata kupona kwao wamekuwa wakichukua muda mrefu tofauti na wengine.

Kuna ambao hawajapata kabisa matatizo haya, hawa wengine wao ni wale ambao wameshapata chanjo ya Covid -19.

Hata kama wapo ambao wameshachanja, nimeeleza hapo juu kuwa hawakuteseka sana na maumivu ya ugonjwa, kukaa nyumbani siku kadhaa bila kwenda kutafuta riziki, pia kuchua muda mrefu kupona.

Kwa maana hiyo, ni kwamba wakati kumeonekana kuna mlipuko wa changamoto ya mafua na homa kali, huu ndiyo wakati wa kukimbilia kwenye vituo mbalimbali vilivyowekwa ili kupata chanjo ya Covid - 19.

Wachezaji soka wengi kabla ya ligi kuu kuanza wakiwamo wa Simba wamechanja, lakini hata baadhi yao ambao wamepata maambulizo na kutocheza mechi dhidi ya Kagera Sugar Jumamosi iliyopita, waliendelea na mazoezi kama kawaida, na kuna timu zingine, zikiwamo Azam, Yanga, Mtibwa Sugar zilikuwa na wachezaji wenye matatizo hayo, lakini waliendelea kucheza.

Ni kwa sababu miili yao ina kinga zaidi. Kama isingekuwa hivyo, sidhani kama wangeweza. Wangekuwa wamelala vitandani kama wengine ambao hawajapata chanjo tunavyowaona.

Kwa maana hiyo sasa Watanzania tujifunze kutokana na hili lililotokea. Chanjo ni muhimu kwa Watanzania wote. Inawezekana kabisa kuwa asilimia 90 ya Watanzania wote wangekuwa wamepata chanjo, changamoto hii isingejitokeza kwa ukubwa huu unaoonekana.

Binadamu siku zote hujifunza kutokana na makosa, lakini inatakiwa Watanzania wanasikosee tena, wahimizane kwenda kuchanja, ili kama kuna tatizo lingine mbele ya safari likute karibuni wote wako vizuri, wameshachanja na wana kinga thabiti mwilini.

RIPOTI MAALUMU

# NEMC & wakazi: Maji ya mgodini yamejaa sumu

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

KWA Wilaya ya Tarime na hususan mazingira ya Nyamongo, kwa sura ya kwanza 'wamebarikiwa' kuwa na uwekezaji mkubwa wa kigeni, Mgodi wa North Mara unaozalisha dhahabu, wenye umri wa miongo miwili sasa.

Lakini katika sura ya pili, mgodi huo ambao zamani uliitwa kwa jina la Nyamongo, kiafya, kimazingira, kiuchumi na hata kijamii sasa umedumu kuwa shubiri kwa wakazi wa jirani, huku majibu ya kinachowasibu yakiwa na sura zote za kitendawili.

Shida kuu iliyotawala nyanja hizo zote, ni maji yatokayo mgodini na kuwafikia wakazi, imewaingiza kwenye mtihani mkubwa kiafya yakiwa na sifa kadhaa za madhara, kwanza yako tofauti na rangi ya maji mengine, yana weupe.

Pia yanalalamikiwa na wenyeji huku Nipashe nayo ikishuhudia kwa sifa; ukipikia chakula hakiivi, ukiyaoga mwili unapauka, yakigusa maziwa yanachacha, wanyama wakiyanywa wanadhurika, hata kufa.

Ni hali ambayo Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) baada ya kuwasilishiwa malalamiko, lilichukua hatua ya kutaka kuthibitisha ukweli huo kitaalamu, nalo limerudi na majibu 'maji yana sumu'.

Nipashe iliyokuwapo eneo hilo wiki kadhaa zilizopita, ilielezwa na mmoja wa wakazi, Mwita Kisiri, mkazi wa mahali huko, anayelalamika kudhurika na maji yanayotiririka kwenye Mto Tigiti ulioko jirani na mgodi huo, akitamka:

"Kuna wenzangu wanapata madhara sasa, ila mimi nilinawa maji tangu mwaka 2003 hadi leo naendelea kupata madhara. Vipele vinatoka mwili mzima na ngozi kubabuka, sasa sijui ndani ya mwili kuna shida kubwa kiasi gani?"

Kisiri analalamika hali hiyo ya kiafya imeshamdhuru katika sura tofauti za kimaisha, ikiwamo kushindwa kumudu kutia huduma kwa familia yake kwa kuwa muda mrefu huwa ni mgonjwa.

Analalamika uwezo wake wa kujitibu kwa sasa ni mdogo, akisema kwa mara ya mwisho alipata matibabu mwaka 2003 katika Hospitali ya Wilaya ya Bunda, alikogundulika ameathirika na sumu.

Mkazi huyo anasimulia ni matibabu aliyoyapata na wenzake kwa msaada wa mgodi. Anafafanua: "Mimi napata shida na kuna wengine wengi wanaendelea kupata shida kutokana na kutumia maji yenye kemikali."



Mkazi wa Nyamongo, Mwita Kisiri, akizungumza na mwandishi wa Nipashe (hayupo pichani) hivi karibuni namna alivyopata madhara mwilini baada ya kuoga maji yenye sumu kwenye Mto Tigiti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**UCHUNGUZI ULIVYOFANYIKA**

Diwani wa Viti Maalum Tarafa ya Ingwe wilayani Tarime, Eliza Malembera, anasema tatizo la maji yenye sumu katika mji wa Nyamongo ni la muda mrefu.

"Walikuja kuchunguza haya maji tunayotumia, wakachanganya maji na maziwa wakachemsha maziwa yakaganda na ndipo Naibu Waziri (Mbunge wa Tarime, Mwita Waitara) aliagiza uchunguzi zaidi wa NEMC," anasema.

Eliza anaendelea kuwa wataalamu wa NEMC walifika katika maeneo yenye maji yanayotiririka na wakachukua sampuri lakini akaeleza kwamba wao wakazi hawajarejeshewa majibu kwa takriban miezi sita sasa.

Ofisa Uhusiano wa Barrick North Mara, Gilbert Mworia, anapotafutwa na Nipashe kuzungumzia suala hilo, anajitetea kwamba mgodi umechukua hatua kukabiliana na baadhi ya mambo inayonyoshewa kidole ili kudhibiti athari za kiafya na kimazingira jirani.

Anataja mojawapo ni kudhibiti maji yenye kemikali kutoka kwenye bwawa lao kuingia kwenye makazi na mito jirani, akisisitiza limefanyiwa kazi kikamilifu.

Ili kupata undani wake, Nipashe ilimfuata Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, anayeeleza majibu ya awali ya vipimo vya sampuli walizozichukua kwenye maji ya Nyamongo yanaonyesha kuwapo kwa sumu inayowaathiri viumbe.

Kwa mujibu wa Dk. Gwamaka, kuna kiwango kikubwa cha tindikali, akiwa na ufafanuzi: "Tumebaini kulikuwa na kiwango kikubwa cha sulphate, nitrate na acidic (tindikali) tofauti na viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS)."

Anaeleza hatua inayochukuliwa hivi sasa dhidi ya malalamiko yaliyoko Nyamongo, imetumwa timu ya wataalamu kusimamia udhibiti wa vyanzo vya madhara hayo kutoka mgodini kwenda kwenye makazi.

"Kuna timu inaenda kusimamia utekelezaji wa makubaliano kati ya mgodi na serikali kuhusu kudhibiti uchafuzi wa mazingira," anabainisha.

Mkurugenzi huyo anafafanua kwamba mikakati inayofanyika ina sura kuu mbili, mosi kudhibiti maji yanayotoka kwenye bwawa la topesumu.

Pili, anafafanua kwamba kemikali zinazotokana na miamba michafu ambayo imekusanywa na haikutoa dhahabu, yenye kawaida inapokaa muda mrefu inatiririsha maji yenye kemikali.

Dk. Gwamaka anasema wataalamu wao pia wanakwenda kufanya uchunguzi kuyabaini maeneo yanayopitisha maji hayo kutoka kwenye mgodi ili yazibwe kwa lengo la kuzuia maji hayo kuingia kwenye vyanzo vya maji safi vinavyotumiwa na wananchi.

**HATUA ZA UTATUZI**

Mbunge wa Tarime, Mwita Waitara, anaungana na Diwani Eliza kukiri kuwa tatizo la maji kudaiwa kuwa na kemikali kwenye eneo la Nyamongo ni la muda mrefu na serikali inaendelea kulifanyia kazi.

Waitara ambaye ni Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, anabainisha kuwa mbali na serikali kuagiza NEMC wapime maji hayo, upo mkakati unaofanyiwa kazi wa kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria hadi Nyamongo na mji mzima wa Tarime ili wananchi waachane na matumizi ya maji yaliyoathiriwa kutokana na shughuli za mgodi.

"Kuna mikakati ya muda mrefu na mfupi. Wakati serikali inatekeleza mpango wa kutoa maji Ziwa Victoria, tayari kuna maagizo ya mgodi wa North Mara kusambaza maji safi kutoka katika visima vyao vya ndani ya mgodi," Waitara anasema.

Mkuu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) Mkoa wa Arusha, Wakili Hamisi Mayombo, anasema kwamba kwa muda mrefu wamekuwa wakifuatilia kero zinazowakabili wananchi wa Nyamongo.

"Kero nyingi za wakazi wa Nyamongo bado hazijapatiwa ufumbuzi lakini tuna imani na serikali, tunaamini zitatatuliwa," alisema.



Sehemu ya mifugo 36 iliyoripotiwa kufa Aprili mwaka jana, katika Kijiji cha Kewanja kilichoko Nyamongo wilayani Tarime baada ya kunywa maji yanayohofiwa kuwa na kemikali za sumu zinazotokana na maji yanayotumika kusafisha mawe ya dhahabu. **PICHA: MAKTABA**

# Wabadhirifu fedha za miradi waonywa

**Na Marco Maduhu,**
KISHAPU

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEM), Dk. Festo Dugange, ameonya ubadhirifu wa fedha kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Ametoa onyo hilo jana wakati akikagua upanuzi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Negezi na ujenzi wa vyumba vya madarasa wilayani Kishapu.

Dugange alisema serikali imetumia fedha nyingi kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, hivyo wanataka kuona miradi hiyo inajengwa kwa kiwango bora na mwonekano wa thamani ya fedha na kusitokee ubadhirifu hata wa senti moja.

"Nimeona ujenzi wa upanuzi wa kituo hiki cha afya, kwa kweli ubora wake ni wa hali ya juu, ila natoa onyo kusitokee ubadhirifu wa fedha yoyote ile, ili majengo haya yawe bora na yatoe huduma kwa muda mrefu na kuokoa afya za wananchi.

"Ujenzi wa kituo hiki cha afya utakuwa msaada mkubwa kwa wananchi wa Negezi na kata nzima ya Ukenyenge, kituo kitakuwa na huduma ya upasuaji na kuepusha kinamama wajawazito kwenda kupata huduma za uzazi umbali mrefu," alisema.

Naibu Waziri huyo pia alipongeza ujenzi wa vyumba vya madarasa wilayani humo ambao upo kwenye hatua nzuri ya ukamilishaji, huku majengo mengine yakiwa yameshakamilika na kuwekwa madawati.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, akitoa taarifa ya ujenzi wa Kituo cha Afya Negezi, alisema walipokea fedha Sh. milioni 250 na ujenzi wake upo katika hatua ya upauaji.

Mkude alisema wanatarajia kukamilisha ujenzi huo mwezi ujao ili Februari kianze kutoa huduma kwa wananchi.

Pia alibainisha walipokea fedha Sh. bilioni 1.9 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 97, ambapo sekondari wanajenga vyumba 81 na shule shikizi madarasa 16.

Baadhi ya wananchi wa Kishapu, akiwamo Sophia Andrew, waliipongeza serikali kwa ujenzi huo wa kituo cha afya, wakieleza kuwa kinamama wajawazito watakuwa wakipata huduma karibu na kuacha kutembea umbali mrefu kwenda Hospitali ya Wilaya na ya Rufani mkoani Shinyanga.



Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dastani Kyobya (katikati), akishiriki pamoja na wananchi katika maandalizi ya awali ya ujenzi wa sekondari mpya ya Kata ya Mtonya iliyoko Manispaa ya Mtwara Mikindani, ambao umeanza rasmi jana, aliwasihi wananchi wa kata hiyo kushiriki kikamilifu ujenzi wa sekondari hiyo ili iweze kukamilika kwa wakati. PICHA: HAMISI NASRI

## ALAF yatia mkono kukuza Kiswahili

**Na Christina Mwakangale**

KAMPUNI ya ALAF Limited imetoa ufadhili wa masomo wa Sh. milioni 10.4 kwa wanafunzi watatu wa Shahada ya Umahiri katika Kiswahili, ikiwa ni mkakati wa kuikuza lugha hiyo ndani na nje ya nchi.

Walionufaika na masomo hayo ni Ester Mgidula, Consolatha Mizimbi na Sophia Kusaga, ambao wote ni wahitimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Akikabidhi hundi ya mfano kwa wanafunzi hao chuoni huko mkoani Dar es Salaam juzi, Meneja Rasilimali Watu wa kampuni hiyo, Jumbe Onjero, alisema lugha ni kiunganishi katika kukuza uchumi nchini, hivyo ipo haja ya kukiendeleza Kiswahili ambacho hutumika kwenye shughuli za uzalishaji kila siku.

"ALAF imekuwa ikijihusisha na utoaji tuzo za fasihi ya Kiswahili kwa takriban miaka mitatu, UDSM wamekuwa wadau muhimu sana katika mchakato wa utoaji wa tuzo hizo.

"Ili kuhakikisha tunakitangaza Kiswahili, tunatoa Sh. milioni 3.4, jumla Sh. milioni 10.4 kwa kila mwanafunzi kusoma shahada hii," alisema Onjero.

Alisema wanafunzi hao watumie fursa hiyo kulingana na malengo kwa kufanya juhudi kwenye masomo ili kukuza, kukiendeleza Kiswahili ambacho huchangia kujenga undugu hata nje ya mipaka.

Kaimu Naibu Makamu Mkuu wa UDSM (Taaluma), Prof. Nelson Boniface, alisema ni heshima kwa chuo hicho na maendeleo ya lugha hiyo baada ya wanafunzi wahitimu kunufaika na mpango huo.

"Wengi wangetamani kupata fursa hii, itumieni vizuri kufikia malengo yenu, chuo, kampuni na taifa. Hii ni mara ya tatu kampuni hii kufadhili masomo kwa wanafunzi wahitimu wa chuo hiki," alisema Prof. Boniface.

Ernesta Mosha, Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), ambaye amemaliza muda wake, alisema wanafunzi hao waliopata ufadhili huo ni kutokana na kuwa na vigezo ikiwamo ufaulu ambao ulikuwa wa juu kulinganishwa na wengine.

Ester Mgidula, akizungumza kwa niaba ya wenzake, alisema anaishukuru kampuni hiyo pamoja na UDSM kutambua umuhimu wa lugha hiyo na kuahidi kuwa mabalozi wazuri wa Kiswahili.

# TCB yagawa miche chotara ya kahawa

**Na Thobias Mwanakatwe**

BODI ya Kahawa (TCB) imeanza kutekeleza mkakati mahususi wa nchi wa kuzalisha tani 300,000 za kahawa ifikapo 2025 baada ya kuzindua ugawaji miche bora chotara ya kahawa milioni 3.048 kwa mikoa ya Songwe, Mbeya, Rukwa na Katavi.

Mkakati huo ulizinduliwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, katika kituo cha utafiti wa zao la kahawa nchini (TaCRI) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kilichoko Mbimba wilayani Mbozi.

Akitoa taarifa ya mkakati huo, Meneja wa Kanda kutoka TCB, Sijali Bowa, alisema mkakati huo ni endelevu na unalenga kufanikisha malengo ya serikali ya kuzalisha tani 300,000 za kahawa ifikapo mwaka 2025.

"Kwa kupitia mradi wa Agri-Conect tunatarajia kuongeza uzalishaji zaidi ukilinganisha na hali ya sasa ambapo tunazalisha kiasi cha tani 70,000 tu kwa mwaka, hivyo ni jukumu la wadau wote wa tasnia ndogo ya kahawa kuhakikisha malengo ya serikali yanatimia," alisema Bowa.

Alisema mradi huo unafadhiliwa kwa pamoja na wadau mbalimbali ikiwamo Umoja wa Ulaya (EU), TCB kupitia ruzuku ya serikali kuu, halmashauri za mikoa inayolima kahawa kwa mikoa ya Nyanda za Juu, AMCOS, wakulima wakubwa na wadogo.

"Zoezi hili tunatarajia kuwa na faida kubwa kwani mbali na kugawa miche bora chotara ya kahawa, lakini tunatarajia kugawa miti ya kivuli na mbao 14,760, ikiwamo miti ya matunda 15,186," alisema.

Baada ya kuzinduzi ugawaji huo wa miche, Mgumba aliwataka wakulima kufuata kanuni bora za utunzaji ili miche hiyo ilete tija kwenye uzalishaji wa kahawa.

Mgumba alisema hali ya uzalishaji wa kahawa kwa mkoa wa Songwe tija yake bado ni ndogo ambapo mti mmoja hutoa gramu 200 tu za kahawa tofauti na nchi za Brazil na Vietnam ambapo tija ni kubwa kwa kuwa mti mmoja hutoa kati ya kilo 2.5 hadi kilo tano.

Mgumba alisema licha ya tija kuwa ndogo bado zao hilo limebaki kuwa mhimili wa mapato ya Mkoa wa Songwe ambapo kwa msimu wa mwaka jana, zao hilo liliuingizia mkoa huo Sh. bilioni 54.

Alizitaka halmashauri za wilaya zinazolima zao la kahawa kurudisha sehemu ya faida wanazopata kama kodi kutoka kwenye kahawa ili zitumike kuzalisha miche bora ya kisasa.

"Hapa niipongeze Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kwa kuchangia kiasi cha Sh. milioni 96 kwa kituo cha TaCRI, lakini nitumie fursa hii kuzitaka halmashasuri zingine nazo kufanya hivyo ili kuongeza tija," aliagiza.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Songwe (SORECU), Royd Mkisi, alisema upatikanaji wa miche bora kutasaidia kuongeza uzalishaji kwa wakulima kwa kuwa wengi bado wana miche ya zamani.

# Wasaliti CCM wasamehewa

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

HALMASHAURI Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, imeridhia kuwasamahe wanachama wake wote waliokuwa wamesimamishwa uanachama kutokana na makosa mbalimbali ikiwamo kukisaliti chama katika uchaguzi mkuu uliopita.

Uamuzi wa kuwasamehe wanachama hao ulitolewa jana mjini Masasi na wajumbe wa kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Masasi kilichofanyika katika ukumbi wa zamani wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

Kikao hicho kililenga kupokea taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho kwa kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka huu.

Awali, akitoa mapendekezo hayo ya kuwasamehe baadhi ya wanachama wake katika kikao hicho, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Masasi, Edward Mmavele, alisema lengo kuu la kuwasamehe wanachama ambao walisimamishwa uanachama kwa makosa mbalimbali, ni kukijenga chama.

Mmavele alisema hakuna sababu yoyote kwa sasa ya kuendelea kuwaacha nje ya chama wanachama hao kwa kuangalia yale walioyafanya huko nyuma kwa sababu chama kwa sasa kinapaswa kuangalia yajayo.

"Hata vitabu vya dini vimehimiza kusamehe sasa, sisi nani tushindwe kusamahe? Ninajua wapo ambao hawatokubaliana na jambo hili lakini jiulize wewe haujawahi kufanya kosa na ukasamehewa? Ninaomba tuwasamehe," alisema Mmavele. Alisema kuwa licha ya maazimio ya halmashauri kuu ya kuwasamehe wanachama hao, wanapaswa kufikishwa katika kamati ya siasa ya wilaya kuhojiwa ili kamati ijiridhishe makosa hayo.

Wakichangia hoja hiyo baadhi ya wajumbe wa kikao hicho, akiwamo Victor Mahelela, walisema hatua hiyo ni mzuri kwa kuwa itasaidia kuvunja makundi yaliyopo yaliyoibuka kipindi cha uchaguzi.

Mjumbe mwingine, Dogras Mkapa, alisema ni wakati wa kujifunza sasa kwa wanachama hao ambao walisimamishwa wanachama kwa kutofanya tena makosa yao. Katibu wa CCM Wilaya ya Masasi, Didas Zimbihile, alisema kuwa halmashauri kuu ni chombo kikubwa cha uamuzi, hivyo kama inafikia uamuzi huo wa kuwasamehe wanachama hao, ni jambo la busara ndani ya chama.




Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima ya Taifa (NIC), Dk. Elirehema Dorie (katikati), akijiandaa kujaza mafuta kwenye gari ya Gracian Chilewa (kushoto), aliyekata bima kubwa kupitia shirika hilo, ikiwa ni uzinduzi wa promosheni ya Jikave na NIC iliyofanyika jana Dar es Salaam kituo cha mafuta cha Puma - Fire. Wateja 500 watapatiwa kuanzia lita 5 hadi 100 za mafuta kutegemea kiasi cha ada ya bima watakacholipa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanane wasimamishwa tuhuma kuomba rushwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAZIRI wa Madini, Dk. Doto Biteko, amewasimamisha kazi maofisa madini wanane wanaofanya kazi katika masoko ya madini kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya kuwaibia wachimbaji wadogo, wizi wa mirabaha ya serikali na uchukuaji wa rushwa kutoka kwa wafanyabiashara wa madini.

Kati ya watumishi hao, wanne wanatoka katika soko la madini wilayani Kahama mkoani Shinyanga na wanne wanatoka katika masoko ya madini Mbogwe na Chato mkoani Geita huku watatu wakiwa katika uchunguzi wa kubaini ukweli wa tuhuma dhidi yao.

Dk. Biteko aliwasimamisha kazi watumishi hao jana katika kikao cha wadau, wachimbaji wadogo na wafanyabiashara wa madini kutoka mikoa 10 ya kimadini nchini, uliofanyika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga.

Lengo la kuitishwa kwa kikao hicho ni kujadili kero zinazowakabili wanaojihusisha na eneo hilo na ukuaji wa biashara zao.

Aliwataja baadhi ya watumishi hao kuwa ni Joseph Mlimi, Mchumi Salumu, Magreth Manamba, Irene Matwe, Andrew Fabiani, Abdallah Mwakidinda, Deogratius Subaila na kwamba wengine waliobaki atakabidhi orodha kwa maofisa madini wa mikoa ili waangalie namna ya kuwashughulikia.

"Kuna mfanyabiashara soko la madini Kahama alifanya uzembe wa kujitakia na tukamtoza faini ya Sh. milioni tatu, lakini maofisa wetu walizunguka nyuma na kumfuata na kumwambia wao ndio wamemtetea na kutozwa kiasi hicho na akawapatia Sh. milioni 20 na tulizifuatilia walizirejesha," alisema.

Dk. Biteko aliongeza: "Inasikitisha sana mtumishi wa umma bado hajathibitishwa kazini anajihusisha katika vitendo vya wizi wa madini na upokeaji wa rushwa kutoka kwa wafanyabiashara wetu.

"Licha ya ukweli kwamba tuna watumishi wachache, hawa tutawaondoa kazini na kuomba kibali cha kuajiri wengine wapya."

Alisema kuwa watoroshaji wakubwa wa madini walikuwa wafanyabiashara na wachimbaji wadogo lakini kwa sasa baadhi ya watumishi wa sekta ya madini, ambao sio waadilifu, wanajihusisha katika vitendo hivyo ambavyo vinasababisha serikali kukosa mapato yake.

Dk. Biteko alimtaka Kamishna wa Tume ya Madini, Janeth Rubeni, kuhakikisha anaunda kamati ya uchunguzi ambayo itawahusisha kamati ya ulinzi na usalama, kuchunguza tuhuma hizo zinazowakabili watumishi wanane waliosimamishwa kazi katika mikoa ya Shinyanga na Geita.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alisema maagizo ya waziri ya kuwasimamisha kazi watumishi wa sekta ya madini yako sahihi na atahakikisha anayasimamia ili kuwe na ufanisi wa kazi katika usimamizi wa masoko ya madini.

Mjema alitoa onyo kwa watumishi wa serikali wenye tabia ya kufanya kazi kinyume cha taratibu za kazi, akiwataka kuacha tabia hizo mara moja na kwa mtumishi ambaye atashindwa kubadilika, aache kazi mara moja kabla hajachukuliwa hatu za kisheria.

Mwenyekiti wa Soko la Madini, Mbogwe Joseph Malimi, alisema soko hilo halina ofisa wa kuhakiki mizigo yao kabla ya kusafirishwa, hali ambayo inawafanya kumpigia simu wakati ukaguzi ilhali anatakiwa kuwapo muda wote sokoni.

# Kibaha yakamilisha ujenzi madarasa 17

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

HALMASHAURI ya Mji wa Kibaha imekamilisha vyumba vya madarasa 17 kati ya 47 vinavyojengwa kwa fedha za UVIKO-19 ambavyo vinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi huu.

Hayo yalibainishwa jana na Ofisa Mipango Takwimu na Ufuatiliaji wa Halmashauri, Wambura Yamo, alipokuwa akitoa taarifa kwa ujumbe kutoka ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) uliofika kukagua ujenzi wa vyumba 47 vinavyojengwa kwa fedha za UVIKO- 19.

Yamo alisema Sh. milioni 940 zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kujenga vyumba 47 na kwamba Sh. milioni 792.6 zimetumika kukamilisha vyumba 17, huku 30 vikiwa katika hatua za mwisho.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Mshamu Munde, alisema utekelezaji wa ujenzi wa vyumba hivyo unaendelea vizuri kwa kuzingatia viwango vinavyotakiwa.

Munde alisema ushirikishwaji wa kamati zilizoundwa kwa kuhusisha wataalamu na wananchi zimeleta morali katika utekelezaji wa mradi huo wa vyumba vya madarasa.

Akizungumza kwa niaba ya ujumbe wa TAMISEMI, Rashid Maftah alipongeza halmashauri hiyo kwa ushirikiano iliyoonyesha kufanikisha ujenzi wa vyumba hivyo kwa wakati kwa kuwashirikisha wananchi wakiwamo wanawake ambao wameshiriki moja kwa moja kwa baadhi ya kazi.

Maftah alisema mbali na ujenzi huo kuondoa vikwazo vilivyokuwapo awali kwenye shule pia umetoa ajira kwa watu mbalimbali wa halmashauri hiyo. Ramadhani Lutambi, Diwani wa Mailmoja, alisema fedha hizo za UVIKO- 19 katika kata yake zimetumika kujenga vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Sekondari Bundikani.

Lutambi alisema tofauti na ujenzi mwingine unaofanyika mara kwa mara, wakati huu wananchi walioshiriki kujenga wamenufaika kwa kupata ajira kuanzia ngazi ya msingi hadi kukamilika.

Aliishukuru serikali kwa kutoa fedha hizo ambazo zimepunguza kero iliyokuwapo awali kwani kwa sasa wana tarajia kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao wamechaguliwa.

# Wadai kulazimishwa kuchanjwa corona ndipo wapate matibabu

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

BAADHI ya wakazi wa Ulowa katika Halmashauri ya Ushetu, Kahama mkoani Shinyanga, wamelalamika kunyimwa huduma za matibabu kwenye zahanati ya kijiji hicho hadi wapatiwe chanjo ya corona.

Walitoa malalamiko hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, wa kusikiliza kero za wananchi wa kata ya Ulowa na kuzitafutia ufumbuzi. Mkutano huo ulifanyika katika kijiji cha Kangeme. Mmoja wa wananchi hao, Zawadi Kimisha, alisema katika zahanati hiyo, wananchi wamekuwa wakipata shida kupata huduma za matibabu kwa kulazimishwa wapatiwe kwanza chanjo ya corona.

Tunaomba serikali iliingilie kati suala hili la kulazimishwa kupatiwa chanjo ya UVIKO-19 (corona) ndipo upatiwe matibabu katika zahanati yetu ya Ulowa. Sasa hivi wananchi hatuendi tena kupatiwa matibabu bali tunakwenda katika Kituo cha Afya Mbika umbali wa kilomita 10 sababu ya kuogopa kuchanjwa bila idhini yetu," alisema Kimisha.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kangeme, Sidini Mlangali, aliiomba serikali kulimaza tatizo hilo ili wananchi wawe wanapata huduma za matibabu karibu na maeneo yao na si kwenda vijiji vya jirani. Aliomba wataalamu waweke kambi kutoa elimu ya chanjo ya corona kwa wananchi.

Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Ushetu, Dk. Alphonce Malunde, alikemea suala la kulazimisha wagonjwa kupatiwa chanjo hiyo bila ridhaa yao na kuonya waganga na wahudumu wa afya watakaobainika kufanya hivyo, watachukuliwa hatua za kinidhamu.

"Maelekezo ya serikali ni kwamba chanjo ya UVIKO-19 ni hiari ya kila mtu kuipata na si kulazimisha, hivyo naagiza madaktari na wahudumu wa afya, mfuate maelekezo na si kujiamulia mtakavyo. Tabia hiyo muiache mara moja, toeni huduma za matibabu kwa wananchi bila masharti," alisema Dk. Malunde.

Mbunge Cherehani kwa upande wake, aliwataka watumishi wa afya wawe wanatoa elimu ya chanjo ya UVIKO-19 kwa wagonjwa, ili wafahamu umuhimu wake, ndipo wawachanje kwa hiari yao wenyewe na siyo kuwalazimisha.

Alisema wananchi wengi wa maeneo ya vijijini hawana elimu ipasavyo ya chanjo hiyo, hivyo wakipata vizuri hakuna haja ya kulazimisha tena kwa kuwa kila mmoja atafahamu umuhimu wake na atakwenda kwa hiari yake kuchanjwa.

Katika hatua nyingine, Cherehani aliahidi kutatua changamoto kwa wananchi hao likiwamo suala la huduma ya umeme, miundombinu ya barabara, maji kwa kuchimba visima virefu pamoja na upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa bei nafuu.



Mkuu wa Kituo cha Polisi Sirari mkoani Mara, SSP Ukulule, akiwasha moto ,magunia 89 ya bangi ambayo yalikamatwa Sirari yakisafirishwa na mtu aliyedaiwa kuwa raia wa Kenya baada ya mtuhumiwa huyo kuhukumiwa kifungo cha miaka 20 jela. **PICHA: SAMSON CHACHA**

# Shehena ya mionzi yarejeshwa ilikotoka

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TUME ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Mionzi ya Nyuklia Kenya (KNRA), imeamuru shehena yenye namba TCKU3337296 iliyokuwa inaingia Tanzania ikiwa na viasili vya mionzi ya nyuklia, kurejeshwa ilikotoka.

Shehena hiyo ilikuwa kwenye meli ya MV SEAGO PIRAEUS VOY 174S ikisafirishwa kuja Tanzania kupitia Bandari ya Mombasa.

Kupitia taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TAEC, Dk.Justin Ngaile, tume hiyo ilibainisha kuwa kabla ya kuzuia shehena hiyo na kuamuru kurejeshwa ilikotoka, walipata taarifa kupitia vyombo mbalimbali vya Kenya kuhusu shehena hiyo na kuwasiliana na KNRA ili kubaini ukweli.

"Tulipowasiliana na hawa wenzetu KNRA Desemba 21, mwaka huu, walithibitisha taarifa hizo za kweli na tayari mamlaka ilichukua hatua stahiki na shehena kuamriwa kurejeshwa ilikotoka," ilibainishwa katika taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa Dk. Ngaile, walipata taarifa kuwa Desemba 22, mwaka huu majira ya saa 6:30 usiku, meli hiyo ilitia nanga Oman katika Bandari ya Salalah.

Alisema TAEC imewaomba Watanzania kuondoa hofu kuhusiana na taarifa hizo kwa kuwa shehena hiyo haikufanikiwa kuingizwa nchini.

Hata hivyo, alisema serikali iko macho na imejipanga vyema katika udhibiti wa uingizaji vyanzo vyote vya mionzi kupitia bandari na sehemu zote za mipaka nchini.

## Aagiza wanufaika TASAF walipwe kabla ya Krismasi

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, amewaagiza waratibu wa Mpango wa Mfuko wa Kusaidia Kaya Maskini (TASAF), mkoa na taifa kuhakikisha wanufaika wa mpango huo wanapewa fedha zao kabla ya Sikukuu ya Krismasl.

Waziri Mchengerwa alitoa agizo hilo wilayani Uvinza akiwa kwenye ziara yake ya kikazi na kuwatembelea baadhi ya wanufaika wa mpango huo kujionea namna fedha hizo zilivyo wasaidia kuondokana na umaskini.

"Tuhakikishe fedha hizi zimetoka haraka sababu fedha tunazo na mimi tayari nimesha kabidhiwa, fedha hizi zilipwe kabla ya Krismasi," alisema Mchengerwa.

Alisema watahakikisha mpango huo unafikia watu wote wenye hali duni kwenye kila kijiji nchi nzima na serikali imedhamiria kufikia kaya milioni 1.5 na kunufaisha idadi ya Watanzania milioni 15.

Aliagiza wataalamu wa TASAF kuwekeza zaidi kwenye utoaji elimu ya ujasiriamali ili wananchi waondokane na umaskini na hatimaye kukua kiuchumi na kuondoka kwenye mpango huo.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa TASAF kijiji cha Kazuramimba Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Ezekiel Honya, alisema mara ya mwisho wanufaika walipata fedha hizo mwezi Juni na Desemba hawajapata tena.

Pia, aliomba idadi ya wanufaika kuongezwa ili kusaidia wananchi kukua kiuchumi kwa kuwa katika eneo lake bado kuna watu wanaostahili kuwa kwenye mpango huo lakini si wanufaika.

Stelia Henga ni binti ambaye wazazi wake wote wana ulemavu ambao walikuwa wakiishi katika umaskini, lakini baada ya kuingia katika mpango huo anaeleza wamejenga nyumba ya bati na kutoka kwenye nyumba ya nyasi waliyokuwa wakiishi pamoja na kupata mtaji unaowawezesha kuendesha maisha.

"Tunashukuru mpango huu kwa kweli umetusaidia sasa tunaishi katika nyumba ya bati," alisema Stelia.



Ukurasa 12

Azindua msimu uzalishaji akihimiza kilimo bora, ulinzi mbegu kisheria




Ukurasa 13

Kwani Krismasi na Mwaka mpya ni lazima?

BUFE
IJUMAA DESEMBA 24, 2021
Nipashe
MIAKA 60 YA UHURU



Ukurasa 14

Kinamama wakulima Mbozi wakusanyika kujifunza, kisha kushinikiza bajeti kilimo

# TGNP yainoa timu Manispaa Ubungo bajeti mtandao, wanufaika tabasamu

• DED, wasaidizi walikubali darasa...

**Na Yasmine Protace**




TGNP Mtandao ikiendelea na moja ya madarasa yake. **PICHA: MAKTABA**

BAJETI yenye mlengo wa kijinsia, msingi wake ni inayobeba kilio cha wananchi kunufaika na fursa zilizopo katika maeneo yanayowazunguka, hata kuwa mkombozi kwa sura pana ya kijamii.

Katika kuhakikisha inajiandaa na bajeti zenye mlengo wa kijinsia, Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo imejipanga kuyafanyia kazi mafunzo waliyoyapata kutoka kwa wadau, asasi wadau wa jinsia na haki za binadamu, TGNP Mtandao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Ubungo, Beatrice Dominica, anasema ni mafunzo yaliyowajengea uwezo katika kuboresha zaidi masuala ya bajeti yenye mlengo wa kijinsia.

"Tumepatiwa mafunzo mazuri sana ya siku moja kutoka TGNP Mtandao, mafunzo hayo yatawajengea uelewa wa pamoja kwa wakuu wa idara kuandaa bajeti katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023," anasema.

Anaongeza kuwa TGNP Mtandao ipo ndani ya Manispaa ya Ubungo, inakofanya shughuli za kuisaidia jamii katika jinsia na lishe, hivyo ipo tayari kusaidiana na halmashauri katika maeneo hayo na mengine.

Mkurugenzi huyo anasema wameshapata nafasi ya kuomba wasaidiwe katika masuala ya lishe, akifafanua: "Ubungo hatujafanya vizuri katika lishe baadhi ya maeneo. Hivyo, tumepata nafasi ya kuiomba TGNP itusaidie, tutakaposaidiwa watoto wakipatiwa lishe bora, watakuwa na afya bora, pia watakuwa wanafanya vizuri katika masomo yao."

Anaongeza kuwa wanatarajia kuwasiliana na uongozi wa TGNP Mtandao kuwaomba wawaandalie mafunzo katika kikao cha watendaji wa kata ambao watapitisha maandalizi ya bajeti.

Hivyo, anaiomba TGNP Mtandao ishirikiane na watendaji wa kata zake nao wapate elimu ya uelewa wa masuala ya jinsia ili waziingize katika ajenda, pia namna ya kuiingiza katika mipango yao.

"Tupo katika kipindi cha maandalizi ya bajeti. Tunawahimiza wakuu wa idara kuyaingiza yale yote tuliyoambiwa katika mafunzo," anasema.

Anaongeza kwamba kabla ya kuwasilisha bajeti zao, watawasiliana na asasi ya TGNP Mtandao kuona namna gani suala la jinsia limekaa sawa katika mustakabali wa bajeti .

Pia, anatoa wito kwa taasisi katika Manispaa ya Ubungo kwamba, katika kipindi cha kuandaa bajeti kuna mambo mengi ambayo serikali inayafanya, hivyo wanaziomba taasisi zingine zishirikiane na kuangalia namna ya kusaidiana.

Grace Mwanjaga, Mchumi kutoka Halmashauri ya Manispaa Ubungo, anakiri mafunzo waliyoyapata yamezingatia mlengo wa kijinsia, pia wana mwongozo wanaoutumia kutoka TAMISEMI.

"Tunazingatia masuala ya mlengo wa kijinsia katika bajeti," anafafanua, huku Ofisa Elimu Vifaa na Takwimu Sekondari katika Manispaa ya Ubungo, Wema Mwakibinga, akiunga mkono namna mafunzo yanawaongezea uwezo katika uandaaji bajeti ya kijinsia.

Hapo anaoanisha na shida ya ziada kwamba katika Manispaa ya Ubungo, kuna changamoto ya kuwa na vyumba maalumu vya kuwahudumia wasichana.

"Tunatarajia kuanzisha mabweni kwa wanafunzi katika shule ya Goba (sekondari) kidato cha tano kwa kuwajengea mabweni wanafunzi wa kike na kiume ," anasema.

**KUTOKA TGNP**

Deo Tena, kutoka TGNP Mtandao, aliyekuwa mkufunzi katika mafunzo hayo, anasema bajeti yenye mlengo wa kijinsia inalenga kutetea masuala ya wanawake, watoto, wanaume na walemavu.

Anafafanua namna Ofisa Elimu Vifaa na Takwimu Sekondari katika Manispaa ya Ubungo, amesema unapozungumzia bajeti yenye mlengo wa kijinsia haimaanishi kumlenga mwanamke pekee.

Ofisa Tena anaongeza kwamba bajeti hiyo ya kijinsia, malengo yake ni kuwagusa wananchi ikiwamo katika kipengele cha kuwaboreshea maisha na kwamba wao TGNP Mtandao wanashawishi umma kuwa na bajeti yenye mlengo wa kijinsia.

"Nchi yetu inatekeleza malengo endelevu ambayo dira ya mwaka 2025 ni kuondoa tofauti, ubaguzi wa rangi na kijinsia," anafafanua na kuongeza kuwa masuala yanayotakiwa kuwamo kwenye bajeti hiyo ni pamoja na kuzingatia masuala ya kijinsia.

Anataja faida sahihi ya bajeti zenye mlengo wa kijinsia, zinasaidia kupunguza ukosefu wa usawa wa kijinsia katika jamii zote.

Pia, Ofisa huyo wa asasi ya TGNP Mtandao, anataja takwimu katika halmashauri kwamba zinatakiwa zitumike katika kupanga bajeti yenye mlengo sahihi wa kijinsia, kwani mara zote takwimu zinasaidia kuondoa kero katika maeneo husika.

"Zipo halmashauri ambazo zimekuwa zikituhitaji kuwasaidia kuandaa bajeti na tumekuwa tukishirikiana nazo kwa karibu," anasema.

BALOZI WA PAMBA – AGGREY MWANRI

# Azindua msimu uzalishaji akihimiza kilimo bora, ulinzi mbegu kisheria

• Bwana Shamba na pikipiki mpya kukagua tija

**Na Anthony Gervas, Magu**

HADI sasa serikali inaendesha mashamba darasa ya zao la pamba, ikiwa ni sehemu ya hatua za kuhakikisha elimu inawafikia wakulima kuhimiza kulima kwa kuzingatia kanuni za kilimo bora cha kisasa, kupitia mfano wa kilichoko katika shamba darasa.

Vilevile, serikali imewapiga marufuku ulimaji wa kuchanganya pamba na na mazao mengine ya chakula na biashara shambani, yakiwamo mahindi, choroko, karanga, maharage, mtama na mengineyo kinyume cha kanuni za kilimo bora cha zao hilo.

Ni aina ya kilimo kinachotajwa kupitwa na wakati, pia hakina tija. Badala yake kitaalamu wanatakiwa kuzingatia kanuni 10 zilizopo kisheria, ili waweze kuzalisha mazao mengi yenye faida kubwa.

Serikali hivi sasa inahimza wakulima kuacha tabia ya kupanda mbegu za pamba katika hesabu za 'kutupia', mbadala unaoshauriwa kupanda mbegu za mazao katika namna ya kuzingatia vipimo vya umbali maalumu na mistari, badala ya holela, hata kusababisha uzalishaji wa mazao kidogo.



Balozi wa Pamba nchini, Aggrey Mwanri (wa pili kulia), alipokagua mashamba wilayani Kaliua, wakati akiwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, alikostaafu mwaka jana. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### MSIMU WA PAMBA

Balozi wa Bodi ya Pamba Tanzania, Aggrey Mwanri, amezindua msimu wa kilimo cha pamba 2021/22 katika kijiji cha Bugatu kata ya Ng'haya wilayani Magu mkoani Mwanza, huku akitaka kilimo chenye tija kubwa.

Mwanri baada ya kupiga marufuku hiyo ya kuchanganya pamba na mazao mengine, ana angalizo kuwa atakayepatikana, 'serikali itamtazama kwa jicho la dharau' akitamka yeye kazi yake itakuwa kuwachongea wakulima wa aina hiyo katika vyombo vya dola, kurupushani anayoitaja itakuwa 'mwendo mdundo.'

Balozi anachowataka wakulima ni kwamba walime kwa kuzingatia kanuni na vipimo vilivyowekwa kisheria na serikali, huku wakiacha tabia za kuzembea palizi ya mashamba yao wakati wanajitambua walichukua mbegu za mkopo, jambo linaloangukia hatima ya uzalishaji kitaifa kuzorota.

Kipimo ambacho ni matokeo ya utafiti wa wataalamu kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika, kinaonyesha upandaji wa umbali kati ya mbegu moja na nyingine ni sentimita 60 kwa upana wa sentimeta 30 unazalisha miche mingi zaidi ya mara mbili ya kawaida.

> **Kati ya matarajio ya tani milioni moja, tani 500,000 zinatarajiwa kuzalishwa katika mkoa wa Simiyu, wakati zinazosalia kuzalishwa ni katika mikoa mingine.**



Pamba iliyostawi shambani.

### AGIZO LA PM

"Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ameagiza wakulima kulima kilimo chenye tija, bila kuchanganya mazao mengine. Ukikamatwa, utapata adhabu kali, mwaka huu serikali inataka tuzalishe tani milioni moja za pamba kitaifa," anaeleza Balozi Mwanri.

Anafafanua kuwa, kati ya matarajio ya tani milioni moja, tani 500,000 zinatarajiwa kuzalishwa katika mkoa wa Simiyu, wakati zinazosalia kuzalishwa ni katika mikoa mingine, mfano Mwanza katika wilaya zake za Magu, Misungwi, Sengerema na Kwimba.

Mwanri anajigamba kwenye sherehe za uzinduzi huo kwamba safari hii kilimo cha pamba 'watatoboa,' lakini akiwa ana tahadharisha kwa wakulima ambao wamechukua mbegu na kukaa nazo nyumbani bila ya kulima akitaka wazirudishe kabla ya msako wa kubainiwa haujaanza.

Anasema wanayo orodha ya wakulima wote waliochukua mbegu kuandaliwa na kuwekwa hadharani, wakiwamo watakaopatikana wakiuza dawa za kuua wadudu katika maduka binafsi.

Pia, anataja hatua kama hiyo kuwafikia wakulima watakaonyunyizia dawa za pamba kwenye mazao ya chakula, kwamba nao watanasa kwenye sheria nao watakamatwa kutokana na dawa hizo kuwa hatari, ikiwa na sumu kali kwa afya ya binadamu.

### ZAWADI BAISKELI

Wakulima waliolima msimu uliopita kwa kuzingatia kanuni bora na vipimo kutoka vijiji vitatu vya Bugatu, Salama na Mwabulenga, walizawadiwa tuzo ya baiskeli kama vitendea kazi vyao wakati wa kwenda shambani, ambazo walikabidhiwa na balozi huyo, ili kuwapa hamasa pia wakulima wengine.

Kampuni ya ununuzi wa Pamba Alliance Ginneries, imekuwa kinara wa kusambaza mbegu za kilimo kwa wakulima, ambazo Bodi ya Pamba Tanzania, iliamua wakulima wakopeshwe na watauza pamba yao kwa kulipwa fedha tasilimu.

Serikali inasema katika kipindi kilichoko itawawekea wakulima mazingira wezeshi, huku ikiwatahadharisha kukaa chonjo kutokana na mvua kutotabirika kunyesha, hali inayoweza kusababisha hali ya ukame.

### MAOFISA UGAVI

Maafisa ugavi nao wametangaziwa neema ya kila mmoja kupewa kitendea kazi pikipiki mpya, wakati wa kutembelea mashamba kukagua na kuona namna taratibu zinafuatwa za kilimo bora.

Mwanri anawatangazia maafisa hao, vita dhidi ya matumizi mabaya ya pikipiki hizo watakazopewa, zisitumike kuwa boda boda mitaani, bali zifanye kazi ya serikali iliyokusudiwa.

Anasema, vyombo hivyo vya usafiri vitafungiwa mfumo wa kusomeka kila zinakokwenda kufanya kazi na kuonyesha umbali iliotembea.

Kwa mujibu wa Balozi Mwanri, ambaye alistaafu akiwa Mkuu wa Mkoa Tabora, ambako nako ni kinara kwa kulima pamba, anasema serikali imelenga kunufaisha familia za wakulima kupitia kilimo cha pamba, pia halmashauri za maeneo husika kupata mapato ya ndani, akisisitiza: "watu wachape kazi siyo kuishia kulalamika kila siku wakiwa vijiweni."

### OFISA KILIMO MAGU

Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wilayani Magu, Godfreda Masale, anasema katika msimu wa kilimo wa mwaka 2021/22, wilaya hiyo imejiwekea lengo la kulima hekta 18,912 za pamba, ikikusudia kuzalisha zaidi ya kilo milioni 22,000,000, wastani wa kuzalisha wastani kilo 450 kwa kila ekari.

Wilaya hiyo iliomba katika msimu uliopo jumla ya tani 472.03 za mbegu za pamba kwa ajili ya kupanda kwenye ekari 47,280 lakini walipata tani 250, hivyo itashirikiana na Bodi ya Pamba kuhakikisha kila mkulima anapata mbegu bora.

Masale anaeleza lengo lingine, ni kufufua vikosi kazi vya ngazi ya vijiji na kata ili waweze kuwafikia wakulima wengi katika wakati mwafaka, kuendelea kufundisha kwa kutumia njia ya mashamba darasa, kuwajengea uwezo wakulima na uzoefu.

Hatua nyingine ni kusimamia wakulima waweze kutumia kamba walizopewa na wataalamu wa kilimo ili kupanda kwa nafasi ya sentimita 60 kwa sentimeta 30, vikosi kazi navyo vinafuatilia mashamba katika changamoto zinazojitokeza.

Mengine yanatajwa ni kuendelea kufanyika mafunzo rejea kwa moafisa ugani na wagani kazi, kuhusu kanuni za kilimo bora ikiwamo utatuzi wa changamoto zinazowakabili wakulima hao.

### TIJA INAVYOSAKWA

Kampeni za kuongeza tija katika zao la pamba, zinaendelea kufanyika kwenye ngazi za vijiji, kata, tarafa hadi wilayani kupitia vikosi kazi vyake vinavyoendeshwa na wataalamu, pamoja na balozi wa pamba tanzania.

Ili kutatua changamoto zinazojitokeza, Balozi Mwanri anasisitiza kuendelea kutolewa elimu, kufanywa ufuatiliaji wa karibu, kufundisha wakulima kwa kutumia mashamba darasa, kushirikiana na Bodi ya Pamba kuchukua hatua dhidi ya wakulima watakaokiuka sheria, huku wakitafutwa wadau mbalimbali watakaowezesha shughuli za ugani kufanyika kwa ufanisi.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Kwani Krismasi na mwaka mpya ni lazima?






NA JOSEPH KULANGWA
+255 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

KOKOTE uliko kaa kimya kwa dakika moja, uungane na mimi kumkumbuka Rais Dk. John Pombe Joseph Magufuli, kwani huu ni mwaka aliotuacha na sasa mwaka wenyewe nao unajiondokea, lakini tunaendelea kumkumbuka kwa mazuri na hata mabaya aliyoyafanya.

Lakini, kama kawaida yetu sisi binadamu hususan wa Tanzania, tuna utaratibu wa kuachana na mabaya,na kuchukua mazuri ya mtu aliyoyaacha, kwani ndiyo yanayotuwezesha kusonga mbele, kwani mabaya kwanza huwa ni machache, lakini tukiyakumbatia hayana maana.

Dk. Magufuli 'aka' Jiwe, alituachia mengi. Tunaona madaraja aliyojenga, tunaona barabara alizojenga, tunaona masoko na stendi alizojenga, tunashuhudia miradi ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa na serikali iliyopo. Bila shaka angekuwapo, tungesikia majina mengi ya madaraja, barabara na hata masoko na stendi.

Tumshukuru alituachia daraja la Patrick Mfugale pale Tazara, akatuachia daraja la John Kijazi pale Ubungo, zote Dar es Salaam). Kama haitoshi, akatuachia barabara nyingine ya Patrick Mfugale, Chamwino, Dodoma, akatuachia soko la Job Ndugai, Dodoma na 'Tower' la Patrick Mfugale kwenye Uwanja wa Ndege wa Chato.

Tunasubiri sasa kusikia daraja la pale Aga Khan hospitali linaloishia Coco Beach, Dar es Salaam sasa lina jina la muda la Tanzanite, bila shaka angekuwapo tusingeacha kusikia jina la shujaa mwingine miongoni mwa mashujaa aliokuwa nao enzi zake, ambao ni wengi tu wakujaa na kusaza.

Tuendelee kumwombea kwa Mungu, aendelee kuilaza roho yake mahali pema peponi. Alimaliza kazi yake nzuri na mwendo wake na sasa katuachia tuendeleze kazi na kweli inaendelea. Madege tuliyaona yakinunuliwa na kutua nchini kwa bashasha. Mungu atupe nini kwa neema hiyo?

Mimi namkumbuka sana 'mate'wangu huyo, kwa alivyokuwa akiamua kijasiri, mathalan kufuta sikukuu na fedha kuhamishiwa kwingine kwa maendeleo ya Watanzania. Mnajionea barabara ya Ali Hassan Mwinyi, kuanzia Morocco mpaka Mwenge jijini Dar es Salaam.

Kama haitoshi, mnajionea hospitali ya Uhuru, Dodoma. Vyote hivyo ni baada ya kuamua kuhamisha fedha za sikukuu.

Kabisa na tena ningeweza kupata fursa, ningeshauri kufutwa hata sherehe hizi za Krismasi na Mwaka Mpya, kwa sababu naona kuna wafanyabiashara wanatumia fursa hizo vibaya, kwa kutupandishia nauli za mabasi na bei za vyakula sokoni.

Watu hawa wasiotosheka na fedha sijui wanatutafuta nini? Kupandisha nauli ili tusiende makwetu kuhesabiwa, ndio iweje sasa? Kutupandishia bei za mchele na nyama ili iweje? Nikidhani kwamba wafanyabiashara hawa wangetumia sikukuu hizi kumshukuru Mungu kwa kutoa sadaka, lakini wanafanya kinyume!

Ningekuwa mimi Mungu kanipa neema hiyo kushinda watu wengine katika jamii, ndiyo kwanza ningeshusha bei ya vyakula kwa asilimia 50 na hata nauli kwenye mabasi ningesafirisha watu bure ili kumshukuru Mungu kwa alichonipa.

Lakini, ndiyo kwanza wafanyabiashara wanatumia fursa hii kukomoa masikini sisi ambao kulawali, biriani au pilau ni mpaka sikukuu. Sasa wanataka tusile ubwabwa Krismasi au kuvaa nguo mpya kwa sababu ya tamaa zao!

Ingefaa kwao wafanyabiashara hawa tungewaona wakipunguza tamaa wenyewe na kutoa sadaka kwa Mungu wao, ambaye kafanya hivyo kungewezesha kuwapa neema zaidi, ili kila mwaka nyakati za sikukuu wapunguze tamaa na bei au nauli za mabasi.

Lakini, naamini hata Chifu Hangaya anaweza kulifanya hilo, kwa sababu yeye na JPM waliapa pamoja kutetea Watanzania. La sivyo, basi vyombo vyake vifanye kazi ya kuhakikisha kuwa wafanya biashara waliojaa tamaa kama hawa, wanaacha tamaa zao na kutuuzia vyakula na nguo kwa bei ya kawaida kama wanaona kupunguza ni ngumu kwao. Vinginevyo wabanwe na spana za Dola. Merry Christmass!!

UCHUMI

# Kinamama wakulima Mbozi wakusanyika kujifunza, kisha kushinikiza bajeti kilimo

• Waibua vipaumbele 6 kuinua kilimo • Halmshauri yaanza kuridhia taratibu

**Na Thobias Mwanakatwe,**

**Songwe**

SEKTA kutekeleza azma ya uwajibikaji wa pamoja, wanawake wakulima wadogo zaidi ya 9000 wanaojihusisha na kilimo Ikolojia katika Halmashauri ya Mbozi, mkoani Songwe, wamekutana kupaza sauti zao katika ushiriki na kuchambua bajeti ya kilimo nchini.

Kwenye kongamano la pamoja la siku tatu kati yao, watunga sera (Madiwani), wakiwamo watendaji wa halmashauri katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya Mbozi, chini ya Mwenyekiti wa kongamano, Mkuu wa Wilaya Mbozi, Cosmas Nshenye na kuratibiwa na Shirika lisilo la Kiserikali la MICO lenye makao yake makuu jijini Mbeya.

Wanawake hao wakulima wadogo waliowezeshwa na MIICO mbinu za uchambuzi wa bajeti, chini ya mradi wa Uimarishaji wa Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii katika Sekta ya Kilimo (PSA), wameibua hoja sita wanazotaka Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi na serikali kwa ujumla kuziingiza na kuzipa kipaumbele katika bajeti ya kilimo ya mwaka ujao ni uliopo.

Wanasema wanashawishi vipaumbele hivyo kuongezwa na kupangwa kwenye bajeti ya kilimo, baada ya kuona changamoto katika maeneo ya huduma bora za ugani na vitendeakazi vya maofisa ugani.

Pia wanataja suala la kupima afya ya udongo, bajeti ya ujenzi wa miundombinu, kuhamasisha Kilimo Ikolojia ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.



Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake Wakulima Wadogo Wilaya ya Mbozi,Vaileth Mkoma (mwenye gauni la bluu), akifuatilia majadiliano ya wanakikundi katika kongamano nje ya ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi. **NA MPIGAPICHA WETU**

### MWENYEKITI WA JUKWAA

Mwenyekiti wa Jukwa la Wanawake Wakulima Wadogo Wilaya ya Mbozi,Vaileth Mkoma, anasema wanataka suala la kupima afya ya udongo kupewa kipaumbele, kwa kuwa na mtaalamu wa kupima tindikali iliyoko ardhini na kuwashauri wakulima aina ya mazao na mbolea inayowafaa kufikia tija.

"Tunataka kupima afya ya udongo, ili wakulima waweze kuzalisha kwa tija kwa kuwa katika maeneo yetu sehemu kubwa ya ardhi imechoka haina rutuba," anasema Mkoma.

Mwenyekiti huyo anasema walitaka pia Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi na serikali, kutenga na kuongeza bajeti iwape hamasa katika kilimo ikolojia, wanachotumia mbegu za asili, pembejeo na viuatilifu vya asili, lengo ni kulinda mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

> **"Tunataka kupima afya ya udongo, ili wakulima waweze kuzalisha kwa tija kwa kuwa katika maeneo yetu sehemu kubwa ya ardhi imechoka haina rutuba.**

"Kwenye kilimo ikolojia sisi tunatumia mbinu mbalimbali za asili kama vile majani ya miti ya matwitwi kama mbolea, pamoja na majani ya utupa kutengeneza dawa za kuhifadhi mazao yasibunguliwe na wadudu," anafafanua Mkoma.

Cecilia Mwansembo, mwanajukwaa kutoka kijiji cha Itaka, anasema Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi na mamlaka za serikali, zinapaswa kuendelea kuongeza bajeti katika sekta ya kilimo, kwani bado kuna changamoto kubwa hususani kwenye huduma bora za ugani na vitendea kazi kwa maofisa wake.

Anaeleza majumuisho ya kongamano hilo la siku tatu,. Lina maudhui: "Tumekubaliana serikali ione uwezekano wa kuajiri maofisa ugani zaidi ili kuendana na miongozo ya kada hiyo inavyotaka kwa kila kijiji walau kuwa na ofisa ugani mmoja.

"Hadi sasa kuna baadhi ya kata zenye zaidi ya vijiji vitano vina ofisa ugani mmoja tu, ambaye kwa namna yeyote ile hawezi kutoa huduma bora na yenye tija."

Kuhusu vitendea kazi, anasema maofisa ugani wanakosa vitendea kazi, hata kukwamisha shughuli za uzalishaji akitumia kielelezo: "Mfano, unakuta Ofisa Ugani kwenye kata nzima yuko mmoja na anatakiwa kuhudumia vijiji zaidi ya vitano, lakini hana usafiri.

"Katika bajeti iliyopita tulipigia kelele suala hili la usafiri walau hata kwa pikipiki na tumesikia halmashauri yetu (Mbozi) imefanikiwa kununua pikipiki tano,ambazo zitagawiwa kwa maofisa ugani."

Mwansembo anashauri Halmashauri ya Mbozi, inabuni mbinu za ziada ili kuwezesha upatikanaji nyumba za maofisa hao ugani waishi jirani na maeneo yao ya kazi.

"Tumeona serikali inavyo hamasisha ujenzi wa vyumba vya madarasa na nyumba za walimu, sasa nafikiri mawazo kama hayo yanaweza kutumika katika upatikanaji wa nyumba za maofisa ugani.

### KITUO UTAFITI

Mwenyekiti wa Jukwaa, Mkoma anazungumzia Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Igamba, sasa kimegeuzwa kuwa mabweni ya wanafunzi.

"Katika wilaya yetu ya Mbozi kulikuwa na kituo kimoja cha utafiti wa kilimo cha Igamba na wanajukwaa tulipoenda kukitembelea kwa kweli tulikuta kina hali mbaya sana," anasema Mkoma.

Anakumbusha lengo la kituo ilikuwa kutoa mafunzo kwa wakulima wilayani Mbozi, lakini wanashangazwa kubadilishwa matumizi kuwa mabweni ya wanafunzi. Hali anayotaja kudhoofisha sekta ya kilimo na uzalishaji chakula kitaifa.

Pia, anataja haja ya bajeti kilimo kuwezesha kupatikana ardhi katika vijiji, ili kuanzishwa mashamba darasa.

### UWEZESHAJI WANAWAKE

Ofisa Mradi Uimarishaji wa Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii katika Sekta ya kilimo (PSA) wa shirika hilo lisilo la serikali la MIICO, Gloria Mdindile, anasema mafunzo ya kuwajengea uwezo wanawake wakulima wadogo yameamsha ari katika uzalishaji mali mashambani, wilayani Mbozi na mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, hususani kilimo Ikolojia.

Anasema MIICO ilianza kutoa mafunzo hayo miaka mitano, tangu 2019 hadi 2023 kwa vijiji vitano vya Itaka, Iyula, Idiwili, Zelezeta na Hasamba katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi.

Mdindile anataja manufaa ya mradi huo kwa kusema kuwa, ndani ya miaka mitatu ya utekelezaji mradi huo katika Wilaya ya Mbozi, baada ya wanawake kushiriki katika uchambuzi bajeti, Halmashauri ya Mbozi imeongeza bajeti yake ya kilimo kutoka asilimia 2.5 hadi kufikia asilimia 13 kwa bajeti ya 2021/22.

" Wanawake baada ya kukutana na watunga sera ambao ni madiwani wao wameendelea kupaza sauti zao kwenye bajeti ya kilimo wakitaka ifike asilimia 20 katika bajeti ijayo ya 2022/23 kama miongozo na sera ya nchi inavyosema," anaeleza.

### BAJETI YA HALMASHAURI

Mratibu wa Uchambuzi wa Bajeti kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Albert Chalii, anasema wanawake wakulima wadogo wa Halmashauri ya Mbozi, wamekuwa chachu kubwa ya maendeleo ya sekta ya kilimo.

Anasema katika bajeti ya 2021/22 baada ya kupokea mawazo mazuri ya wanawake wakulima, halmashauri imeweza kuboreshwa baadhi ya mipango yake ikiwemo kuongeza bajeti katika eneo la maofisa ugani, shilingi milioni 19 zilitengwa .

Anasema fedha hizo tayari zipo kwenye akaunti ya Halmashauri na kwa kuanzia wanatarajia kununua pikipiki tano kwa ajili ya kuwagawia maofisa ugani ili kuwarahisishia utekelezaji wa majukumu yao.





Baadhi ya wananchi wakiwa kwenye pilika pilika za kutafuta mahitaji ya sikukuuu ya Krismasi Mtaa wa One Way Jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Dodoma kukabidhi madarasa 601 fedha za UVIKO-19

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, amesema mkoa wake unataraijia kukabidhi vyumba vya madarasa 601 yanayojengwa kupitia fedha za mapambano dhidi ya UVIKO- 19 Desemba 30, mwaka huu.

Mtaka, alibainisha hayo jana jijini hapa baada ya kufanya ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari.

Alisema kutokana na ziara hiyo amebaini kuwa ujenzi wa madarasa unakwenda vizuri na matarajio ya mkoa kukabidhi vyumba vyote ni Desemba 30, mwaka huu.

"Kama mkoa tumeridhika na hatua ya ujenzi ilipofikia na tunataraji kufanya hafla kukabidi vyumba hivi 601 vya mkoa katika wilaya moja ambayo tutaichagua kwa niaba ya mkoa," alisema.

Mtaka aliagiza wilaya zote ambazo zinatekeleza mradi huo kuhakikisha kuwa zinapanda miti katika maeneo ya shule.

"Wakati madarasa haya yanajengwa naomba yaendane na zoezi la upandaji wa miti haiwezakani shule inakuwa na majengo mazuri, lakini maeneo yake yamepauka, lazima kila mwanafunzi apate mti mmoja wa kuutunza," alisema Mtaka.

Vilevile, aliiuagiza uongozi wa Jiji la Dodoma kupitia idara ya elimu kusambaza walimu katika maeneo yenye upungufu.

Alisema hivi sasa yapo maeneo ambayo yana walimu wa ziada ambao hawana kazi za kufanya na badala yake wamekuwa wakigoma kila siku.

"Nimepata malalamiko kuna sehemu walimu wapo wengi hata kufundisha hawafundishi wanabaki kugoma tu, idara ya elimu lazima iwasambaze hawa ambao wamezidi katika baadhi ya maeneo," alisema.

Kadhalika alisema watoto wote wenye sifa ya kwenda shule wanatakiwa kuripoti ifikapo Januari 17, mwakani bila kikwazo chochote.

"Itakuwa ni aibu kubwa kuwa na majengo mazuri na ya kisasa ambayo yanajitosheleza, lakini watoto hawaendi shule, hatutaki kuona watoto wanaonekana sokoni, mitaani pamoja na mashambani au kuwa sehemu ya kutunza familia," alisisitiza Mtaka.

Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, alisema ujenzi wa vyumba vya madarasa hayo umegharimu Sh. bilioni 12.02.

Pia alisema Mkoa wa Dodoma unajenga madarasa 175 kwa ajili ya shule shikizi ambayo yatagharimu Sh. bilioni 3.5.

"Tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan, kwani bila yeye hii ilikuwa ngumu sana kwa kutumia fedha za ndani tu ingetugharimu kiasi cha Sh. bilioni 15.5 hii ingekuwa changamoto kwetu," alisema.

Aliziagiza halmashauri fedha ambazo walitenga kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya sekondari zielekezwe katika shule za msingi ili kutatua kero iliyopo hivi sasa.

Kaimu Ofisa Elimu Sekondari Jiji la Dodoma, Fredrick Mwakisambwe, alisema kupitia fedha za mapato dhidi ya UVIKO-19 wanajenga madarasa 147.

Mwakisambwe, alisema vyumba vinne ni kwa ajili ya shule shikizi na ujenzi wake utarajiwa kukamilika Desemba 24.

"Madarasa mengi yapo katika hatua za umaliziaji tunatarajia kabla ya sikukuu ujenzi uwe umekamilika katika shule zote ibaki kazi ya kuingiza madawati," alisema.

# Babu mbaroni madai ya kubaka mjukuu wake

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma linamshikilia mzee mwenye miaka 61 kwa tuhuma za kumbaka mjukuu wake mwenye umri wa miaka 11 ambaye ni mwanafunzi wa darasa la nne.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Onesmo Lyanga, alisema tukio hilo limetokea juzi katika Wilaya ya Kongwa na polisi inamshikilia mtuhumiwa huyo kwa tuhuma hizo.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Kamanda Lyanga alisema tukio hilo ni la kikatili na linahitaji kukemewa mbele ya jamii.

"Hii tabia si nzuri inapaswa kuipiga vita ili jamii wakiwamo watoto wawe salama," alisema Lyanga.

Polisi pia inamshikilia kijana wa miaka 30 kwa tuhuma za kumbaka mama yake mzazi mwenye umri wa miaka 75.

Kamanda Lyanga alisema tukio hilo limetokea wilayani Kondoa.

Alisema watuhumiwa wote wamefikishwa mahakamani kutokana na makosa hayo huku wakisubiri mkono wa sheria.

Jeshi hilo pia limemkamata mtuhumiwa akiwa na vipande vitatu vya meno ya tembo vyenye thamani ya Sh. milioni 69 ambavyo alivificha katika begi lake.

Alisema watuhumiwa wote wamefikishwa mahakamani kusubiri mkono wa sheria.

# Serikali haitafunga mipaka wakulima kuuza mahindi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema haitafunga mipaka yake kwa ajili ya kuwazuia wakulima wanaotaka kuuza mahindi yao nje ya nchi.

Hayo yalibainishwa juzi na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa kiwanda cha mbolea kinachojengwa na wawekezaji kutoka Burundi eneo la Nala, jijini hapa.

Bashe alisema, kwa sasa Tanzania ina akiba ya chakula cha kutosha na wafanyabiashara wanaouza nje ya nchi hawatafungiwa mipaka ya kuuza wala kupangiwa bei.

Kadhalika, Bashe aliwataka wataalamu wa utafiti wa kilimo (TARI) pamoja na wataalamu wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula nchini (NFRA), kukaa pamoja na wawekezaji wa kiwanda cha mbolea cha Itracom Fertilizers LTD ili kuweka mpango kazi wa kufanikisha mahitaji sahihi katika matumizi ya mbolea katika kila mkoa na wilaya zake.

Alisema kwa kuwa kiwanda hicho kinategemea kukamilika mwezi Julai mwakani, mipango mikakati hiyo inatakiwa iwe imekamilika mwezi Mei 2022, ili kupunguza changamoto zilizojikeza katika viwanda vingine vya uzalishaji mbolea.

"Tumeona changamoto ya matumizi ya mbolea katika maeneo mbalimbali sana natoa maagizo kwa taasisi ya utafiti wa kilimo na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kukaa pamoja na wawekezaji kutoka Burundi ili kuweka mpango kazi wa kubaini jambo la kufanya katika ufafiti wa mbolea ili kujua ni aina gani ya mbolea inatakiwa na ni sehemu gani.

"Naagiza vikao vyenu vifanyike na ifikapo mwezi Mei mwakani muwe mmeshapata ufumbuzi kwa kuwa changamoto ambazo zimekuwa zikipatikana katika viwanda vingine vya kuzalisha mbolea isije ikajitokeza katika kiwanda hiki," alisema Bashe.

Alisema uzalishaji wa mbolea nchini uwe na malengo ya kujibu mahitaji ya wakulima na ijulikane kuwa mikoa na wilaya zinatofautiana na kwamba ni vyema kubaini mbolea inayofaa kwa lengo la kuboresha kilimo.

Katika hatua nyingine, Bashe alisema asilimia kubwa ya mbolea itayotengenezwa na kiwanda hicho inatokana na samadi na lazima ukusanyaji wa samadi ufanywe na wazawa.

Hata hivyo, Bashe alisema kutokana na wakulima wengi kutumia mbolea ya chumvi imesababisha ardhi kupoteza ubora, kiwanda hicho kitazalisha chokaa kwa ajili ya kuhuisha ubora wa rutuba ya ardhi.

Mwekezaji wa kiwanda hicho kutoka Burundi, Mhandisi Musafiri Dieudonne, alisema ujenzi huo ni mkombozi mkubwa kwa mkulima wa Tanzania na utasaidia kuwatoa katika kilimo cha kujikimu na kufanya kilimo biashara.

Alisema kiwanda kitagharimu Dola za Marekani milioni 180 na kinatarajiwa kukamilika Julai mwakani.

Hata hivyo alisema pamoja na ujenzi wa kiwanda hicho wanakabiliwa na changamoto ya uhaba wa maji na kukatika katika kwa umeme mara kwa mara.





# Polisi yatoa ushauri kuimarisha ulinzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limewataka viongozi wa makanisa kuzitumia Kamati za Ulinzi na Usalama za makanisa kuimarisha ulinzi kwenye maeneo ya ibada wakati wa Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya ili kuepusha vitendo vya uhalifu kwenye maeneo hayo.

Pia, limewataka wamiliki wa kumbi za starehe kutumia walinzi binafsi kuimarisha ulinzi kwenye maeneo yao hasa kwenye maegesho ya magari ili kuwadhibiti wahuni watakaotaka kufanya uhalifu.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya sikukuu hizo za mwisho wa mwaka.

Alisema jeshi hilo limejipanga kuimarisha ulinzi kwenye maeneo yote kwa kuhakikisha wanakuwapo askari wa doria hasa kwenye maeneo ya mikusanyiko yakiwamo makanisa na kwenye kumbi za starehe.

Aliwataka wamiliki wa kumbi za starehe kuzingatia sheria kwenye uendeshaji wa shughuli zao hasa muda wa kufungua na kufunga ili kuepuka mkono wa sheria.

Vilevile, alitaka idadi ya watu wanaoingia kwenye kumbi hizo isizidi uwezo kuepuka madhara ya kukanyagana na baadhi kukosa hewa ya kutosha.

"Tunawashauri pia wazazi kuhakikisha hawawaachi watoto wao kwenda peke yao kwenye matembezi, angalau wawe na mtu mmoja mzima wa kuwalinda ili wasidhurike, na watoto hawaruhusiwi kuingia kwenye kumbi za starehe," alisema Kamanda Matei.

Vilevile, alisema jeshi hilo linaendelea kutoa elimu ya usalama barabarani kwa madereva na watumiaji wengine wa barabara kuzingatia sheria ili kuepuka ajali ambazo zinaweza kugharimu maisha ya watu.

Alisema kwa sasa jeshi hilo limeanzisha utaratibu maalumu wa kuyasindikiza mabasi kutoka stendi kuu ya Mbeya mpaka katika eneo la mpaka zaidi ya kilomita 100.

Aliwataka abiria kuwa wavumilivu kipindi hiki ambacho mabasi hayakimbii kama ilivyokuwa miezi ya nyuma kwa kuwa wameamua kuyadhibiti kwa ajili ya usalama wa wao na mali zao.

"Lakini kwenye maeneo ya miteremko magari yataendelea kupita kwa awamu, magari ya mizigo yatapita peke yake na ya abiria yatapita peke yake hasa kwenye miteremko wa Mbalizi, Mwansekwa, Igawilo na Mlima Nyoka," alisema Kamanda Matei.

Hata hivyo, alisema katika maeneo ya fukwe za Ziwa Nyasa zilizoko wilayani Kyela, jeshi hilo litaimarisha ulinzi ili kuhakikisha madhara hayatokei kwa watu watakaokwenda kupumzika.

Kamanda Matei aliwataka wananchi kusherehekea sherehe hizo kwa amani huku akiwataka wanaokunywa pombe wanywe kiasi ili kuepusha madhara.

Aliwataka wananchi kutoa taarifa kwa jeshi hilo pamoja na viongozi wa serikali endapo watabaini uwapo wa mtu ama kikundi chochote cha watu wanaopanga kufanya uhalifu ili wadhibitiwe kabla hawajatekeleza uhalifu wao.



Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, akiwahutubia wananchi wa Kata za Igale na Iwindi (hawapo pichani) kwenye mkutano wa hadhara kusikiliza kero za wananchi juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wakulima walalamika uhaba wa mbolea

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa Kata za Igale na Iwindi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamelalamikia uhaba wa mbolea katika maeneo yao na bei kuwa juu kwa maelezo kuwa hali hiyo itawasababishia kushuka kwa uzalishaji wa mazao.

Walitoa kilio hicho kwenye mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mbunge wa Jimbo hilo, Oran Njeza.

Walisema wana wasiwasi mwaka ujao kutakuwa na njaa kutokana na watu wengi kushindwa kununua mbolea.

Mmoja wa wananchi hao, Paison Kawongo, alisema kwa sasa mbolea ya kupandia inauzwa kati ya Sh. 115,000 na 120,000 bei ambayo alisema ni kubwa na haijawahi kutokea katika kipindi chote anachojishughulisha na kilimo.

Alisema hata upatikanaji wake ni kwa kiwango kidogo na kusababisha bei kuendelea kupanda na kuwapa wasiwasi wa tija ya uzalishaji kupungua.

Alisema endapo uzalishaji utapungua kuna hatari pia ya kukumbwa na tatizo la njaa pamoja na uchumi wao kushuka.

"Sasa hivi tunahangaika na mabadiliko ya tabianchi ambayo yamesababisha msimu wa mvua kutoeleweka, sasa limekuja tatizo la mbolea, tunashindwa kununua kabisa maana bei ya mahindi tuliyolima msimu uliopita ilikuwa chini sana," alisema Kawongo.

Naye Jerome Shila aliiomba serikali iwe na utaratibu wa kudhibiti bei ya pembejeo zote ili kuimarisha sekta ya kilimo ambayo ni miongoni mwa sekta zinazoliingizia taifa fedha nyingi pamoja na kulihakikishia taifa usalama wa chakula.

Alimwomba mbunge wa jimbo hilo, Njeza kuwasaidia kuwasilisha kilio chao serikalini ili wasaidiwe na ikiwezekana serikali iwaingizie ruzuku kwenye pembejeo ili bei zipunguzwe.

Akijibu malalamiko ya wananchi hao, Njeza alisema ili kuwasaidia wakulima ameshaanza mazungumzo na baadhi ya wadau wanaosambaza pembejeo ili wawasaidie kupunguza bei ya mbolea.

Alisema kuna kampuni moja ambayo ameshafanya nayo mawasiliano na imekubali kupunguza bei kwa asilimia 15 ili badala ya bidhaa hiyo kuuzwa kati ya Sh. 115,000 na 120,000 iuzwe kwa Sh. 95,000 wananchi waweze kumudu.

Alisema serikali pia inaendelea na michakato mbalimbali ya kukabiliana na tatizo la mfumuko wa bei ya mbolea ikiwamo kuwaruhusu wafanyabiashara kuingiza mbolea kwa wingi kutoka nje na kuwashawishi wapunguze bei.

"Ni kweli kwa sasa bei ya mbolea iko juu na hii imesababishwa na tatizo la corona, wamiliki wengi wa viwanda wamepunguza uzalishaji na baadhi wamefunga viwanda, sasa kwa kawaida kitu kikipungua ni lazima bei yake ipande," alisema Njeza.

Aliwataka wakulima kuendelea kuzalisha mazao kulingana na uwezo wao ili wasije wakakosa chakula kwa kisingizio cha kukosa mbolea.

## Walimu wapongezwa shule kushika nafasi ya 14

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMATI ya Shule ya Msingi Uhuru iliyopo katika Kata ya Mwakibete Halmashauri ya Jiji la Mbeya, imewapongeza walimu wa shule hiyo kwa kuwasaidia wanafunzi waliohitimu darasa la saba mwaka huu kufaulu vizuri na kuifanya shule hiyo kushika nafasi ya 14 kwa Jiji.

Walimu hao walipongezwa kupitia hafla maalumu iliyoandaliwa na kamati hiyo juzi iliyoandaa chakula cha pamoja na walimu.

Walisema shule hiyo imepanda kutoka nafasi ya 37 mwaka jana mpaka nafasi ya 14 mwaka huu.

Mwenyekiti wa Kamati ya shule hiyo, Titho Nyondo, aliwapongeza walimu hao kwa ushirikiano waliouonyesha kwenye maandalizi ya wanafunzi hao na kuwasaidia wafaulu vizuri.

"Tumeona tusiishie tu kufurahi tukiwa nyumbani tukaona ni vyema tufurahi pamoja hapahapa shuleni ili tusaidiane na kupanga mipango ya mwakani, hongereni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya katika kipindi chote," alisema Nyondo.

Alisema wataendelea kutoa ushirikiano kwa walimu hao ili kuhakikisha wanafanya kazi katika mazingira rafiki na aliwaomba kuishirikisha kamati hiyo kwenye mambo yote ya maendeleo ya shule hiyo.

Kwa upande wake Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Agnes Mwila, alisema walifanya kazi kwa ushirikiano na kamati hiyo na kuwaomba wajumbe wa kamati hiyo kuendelea kushirikiana nao ili kuendeleza hali ya ufaulu.





## Wamiliki mitandao kijamii walia na tozo za usajili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAMILIKI wa Mitandao ya Kijamii Zanzibar wameomba serikali kupitia Tume ya Utangazaji Zanzibar, kupunguza gharama za usajili wa mitandao hiyo ambayo ni kubwa kulingana na kipato chao.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wamiliki hao walisema kila mwaka wanatakiwa kulipa Sh. 500,000 ili kufanya kazi zao za utoaji wa taarifa kwa jamii kiwango ambacho wamekilalamikia ni kikubwa. Yassir Mkubwa ni miongoni mwa wamiliki wa mitandao hiyo ya kijamii, alisema kuwa bado hali yake ya kiuchumi ni ndogo na gharama ya usajili wa mtandao ni kubwa na kuomba serikali kupunguza kiwango hicho ili vijana wapate fursa ya kujiajiri na kuajiri wengine.

"Sisi tunaotumia mitandao ya kijamii tunachangamoto kubwa kwanza hatuna fedha tunayoingiza zaidi ya kutoa elimu kwa jamii kupitia taarifa mbalimbali," alisema Mkubwa.

Naye mwandishi wa habari wa runinga ya mtandaoni (Zinjibar TV), Safia Hussein, aliomba Tume ya Utangazaji kuwapatia mafunzo yatakayowawezesha kutekeleza majukumu yao na kufikisha taarifa kwa jamii zenye kuleta mabadiliko ya maendeleo na kiuchumi.

Alisema suala la kuzingatia maadili katika kazi ya kuwasiliana na umma katika mitandao ni muhimu huku akiwataka vijana wenzake kujiendeleza kielimu ili wasiachwe nyuma na mabadiliko.

"Mafunzo kwa ajili ya kufahamu makosa ya mitandao ni muhimu katika kipindi hiki ambapo zipo sheria za makosa ya mitandao ambazo tunatakiwa kuzifahamu ili kujiepusha makosa yanayoweza kututia hatiani," alisema.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji wa Tume ya Utangazaji Zanzibar, Suleiman Abdallah Salim, aliwataka wamiliki wa vyombo vya habari hasa mitandao ya kijamii kufika ofisini kwake kwa lengo la kujisajili na kulipa gharama za utendeshaji wa vyombo hivyo.

Alisema kurusha maudhui bila ya kufuata taratibu na sheria zilizopo ni kosa kisheria na tume yake haitosita kuwachukuliwa hatua za kisheria.

Alisema kuwa Zanzibar ina vyombo vya utangazaji 65 ikiwamo mitandao ya kijamii, lakini alishangazwa kuwa vinavyolipa ada ya utangazaji ni vichache na kutoa notisi ya siku 14 kuhakikisha vyombo vyote vinalipa tozo ya utangazaji iliyowekwa.

"Tayari tumeshafanya kikao na wamiliki wa vyombo vya habari ikiwamo mitandao ya kijamii na moja ya changamoto waliyoeleza ni tozo kubwa ya utangazaji nimewaahidi kuwa tutaifanyia kazi," alisema.

Alisema tume hiyo itahakikisha inaboresha mfumo wa ufuatiliaji wa maudhui ya mitandaoni ili kuhakikisha vituo hivyo vinafuata sheria na kanuni za utangazaji.

# Mwinyi avitaka vyuo vikuu kuanzisha programu za kujiajiri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali imeshatangaza dhamira ya kukifanya kisiwa hicho kuwa ni kitovu muhimu cha biashara na teknolojia ya habari katika ukanda wa Afrika Mashariki ili kulifikia lengo hilo vyuo vikuu lazima viwe mstari wa mbele kutoa mafunzo na programu tofauti zinazohusiana na fani hizo.

Dk. Mwinyi alieleza hayo kupitia hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, katika sherehe za mahafali ya 19 ya Chuo Kikuu cha Zanzibar yaliyofanya Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja.

Alivitaka vyuo vikuu na taasisi za elimu nchini kuendelea kuanzisha programu mpya ambazo ni muhimu katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ili kuongeza fursa za ajira.

Alisema vyuo vilivyoko nchini lazima vishike usukani kukuza ubunifu na viwe tayari kushiriki kubuni mipango muhimu ya maendeleo kwa taifa.

Kadhalika alisema kuendeleza uchumi wa buluu ni miongoni mwa vipaumbele vilivyowekwa na serikali, na kuviomba vyuo vikuu viendelee kutoa ushirikiano kwa serikali kwa kuanzisha na kufundisha programu mbalimbali zitakazowezesha kuwa na rasilimali za bahari.

"Lazima tuondokane na hali tuliyonayo hadi sasa hatuna hata chuo kikuu kimoja au taasisi ya elimu ya juu hapa Zanzibar yenye kufundisha programu muhimu zinazohusu uvuvi na uendelezaji wa rasilimali za baharini," alisema Rais Mwinyi.

Vile vile, alivikumbusha vyuo mbalimbali nchini kuendelea kufanya utafiti ili kuiwezesha jamii kutatua changamoto zinazowakabili katika mazingira yanayowazunguka.

Alisema serikali inafahamu kuwa vyuo vingi vilivyoko Tanzania Visiwani na Tanzania Bara, vinakabiliwa na changamoto ya ushindani mkubwa katika kuwavutia na kusajili wanafunzi wapya kulikochangiwa na ongezeko la idadi ya vyuo vikuu nchini.

Alivishauri vyuo hivyo na taasisi zingine za elimu ya juu kubuni vitu vya ziada vitakavyowashawishi wanafunzi wapya wanaotaka kujiunga na vyuo hivyo.

Pia, aliupongeza uongozi wa Chuo Kikuu cha Zanzibar kwa juhudi wanazozichukua kwa kushirikiana na serikali kuandaa wataalamu na viongozi wa ngazi mbalimbali katika kipindi cha miaka 19 tangu kilipoanza kutoa wahitimu baada ya mahafali ya kwanza kufanyika.

Naye Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Abdulkadir Othman Hafiz, alipongeza Serikali ya Zanzibar kwa ushirikiano katika kukiendeleza chuo hicho ambacho kimefanikiwa kutoa taaluma kwa wanafunzi wengi nchini na ukanda wa Afrika Mashariki.

Dk. Abdulkadir alisema tangu kuanzishwa kwa chuo hicho Zanzibar mwaka 1998, kumekuwapo kwa ushirikiano mkubwa kutoka serikalini na kusaidia chuo kufikia maendeleo na malengo kilichojiwekea.

Alisema chuo hicho kitaendelea kutoa taaluma kwa wanafunzi wa Zanzibar na Afrika Mashariki ili kuzisaidia jamii zinazowazunguka.

Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Haroonah Nsubuga, alisema katika mahafali hayo ya 19 jumla ya wanafunzi 617 wamehitimu kupitia fani mbalimbali wakiwamo wanawake 345 kwa ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu.

Prof. Nsubuga aliwakumbusha wahitimu hao kutoridhika na kiwango cha elimu walichokipata na kueleza kuwa kuna haja ya kujiendeleza zaidi kitaaluma kwa ngazi za juu ili kujiweka vizuri katika soko la ajira.



Mtalii kutoka Ulaya akiangalia bwawa la mfugaji wa kasa, Mohamed Mataka, Nungwi, mkoa wa Kaskazini Unguja jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Uchakavu maghorofa wasababisha wakazi kuhamishwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema nyumba za maendeleo za ghorofa zilizoko Kengeja Pemba zipo katika hali mbaya huku wakazi wake wakilazimika kuhamishwa ili kuepuka athari za usalama wa maisha yao.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Riziki Pembe Juma, wakati akitoa ufafanuzi kuhusu hali ya nyumba za maendeleo zilizojengwa na Rais wa Kwanza wa Zanzibar, hayati Abeid Amani Karume, katika miaka ya 1969 ambazo nyingi hazijafanyiwa ukarabati.

Waziri Pembe alisema nyumba za maendeleo zimejengwa miaka mingi na kwa bahati mbaya hakuna matengenezo muhimu yaliyofanywa matokeo yake nyingine zimeharibika kwa kupata nyufa na kuta kupasuka.


Alisema katika nyumba za Kengeja Pemba tayari wakazi wake wamelazimika kuhamishwa kwa sababu zipo katika hali mbaya na wizara imefanya mawasiliano na serikali kuu kuhusu hatima ya nyumba hizo kama kuzifanyia ukarabati au kuzivunja.

"Tumewasilisha maombi yetu serikali kuu kuhusu hatima ya nyumba za maendeleo zilioko Kengeja, Mkoa wa Kusini Pemba, kama tuzifanyie ukarabati au zibomolewe moja kwa moja kwa sababu tayari muda wake wa kuishi umepita," alisema.

Alisema nyumba nyingi za maendeleo zilizoko Pemba zipo katika hali mbaya ya uchakavu ikiwamo Chakechake, Mkoani, Micheweni pamoja na Kengeja.

## HABARI PICHA

# MATUKIO MBALIMBALI YA WIKI




Meneja wa Kampuni ya ALAF, inayotengeneza mabati, Jumbe Onjero (katikati), akimkabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni tatu na laki nne, mmoja wa mwanafunzi kati ya watu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Sofia Kusaga, kwa ajili ya kuwaendeleza kielimu katika lugha ya Kiswahili, hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. PICHA: JUMANNE



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Morilo, akionyesha bastola bandia na baadhi ya bidhaa zilizoibiwa katika maeneo tofauti jana. PICHA: JUMANNE JUMA



Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Sayi Magessa (kushoto), akiteta jambo na Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Maendeleo Afrika WiLDAF, Anna Kulaya, wakati wa kongamano la wadau lililokuwa likijadili utekelezaji wa miaka mitano lililfanyika jijini Dar es Salaam jana. PICHA: JUMANNE JUMA




Mafuriko ya abiria waendao mkoani Kilimanjaro wakiwa katika kituo kikuu cha mabasi wakihangaika kupata usafiri kwenda kula sikukuu ya Krismasi mikoani. PICHA: TUMAINI MAFIE




Mkurugenzi Mtendaji wa LG Electronics Afrika Mashariki, SaNyoung Kim (kulia), na Mkurugenzi Mtendaji wa Garnet Star, Rajesh Nomulwar, ambaye kampuni yake ni wakala wa bidhaa za LG Tanzania wakikata utepe kuashiria uzinduzi wa duka jipya la LG eneo la Morocco jijini Dar es Salaam hivi karibuni. PICHA: JUMANNE JUMA



Meneja Mkuu wa Shirika la Reli TAZARA kwa upande wa Tanzania, Fuad Abdallah, akiwakabidhi walezi wa kituo cha kulelea watoto wenye mahitaji cha Valentine Children's Home, Watawa Lucy Lipenga (kushoto) na Janeth Layi zawadi mbalimbali zilizotolewa na wafanyakazi wa shirika hilo, jijini Dar es Salaam jana. PICHA: JUMANNE JUMA

# HABARI KIMATAIFA

## Marekani yashtuka uhusiano wa profesa wake na China

**Washington,** MAREKANI

PROFESA kutoka Chuo Kikuu cha Harvard, ameshtakiwa kwa kudanganya mamlaka za serikali kuu, juu ya uhusiano wake na serikali ya China na chuo kikuu kimoja cha nchi hiyo.

Charles Lieber, mwenye umri wa miaka 62 ni mtaalamu wa teknolojia ya atomu na mwenyekiti wa zamani wa Idara ya Kemia na Kemibiolojia ya Chuo Kikuu cha Harvard.

Wanabaraza wa mahakama ya serikali kuu mjini Boston walimpata na hatia juzi Jumanne.

Wizara ya Sheria Marekani, ilisema kundi lake la utafiti lilipokea zaidi ya dola milioni 15 kama msaada wa utafiti kutoka Wizara ya Ulinzi ya Marekani na Taasisi ya Afya ya Taifa.

Maofisa wa wizara hiyo walisema wakati huo, Lieber alikuwa ameanzisha maabara ya utafiti wa pamoja wa maswala ya atomu katika Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Wuhan nchini China, bila Chuo Kikuu cha Havard, kufahamu.

Walisema Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Wuhan, kilimlipa Lieber mshahara wa hadi dola 50,000 kwa mwezi na gharama za matumizi ya kila siku za hadi dola 150,000 kwa mwaka, pamoja na dola milioni 1.5 za kuanzisha maabara hiyo ya pamoja.

Wizara ya Sheria ilisema, Lieber pia alikuwa mkandarasi mshiriki katika Mpango wa Vipaji 1,000 wa serikali ya China, unaoajiri wanasayansi wabobezi kutoka nje ya China.

Aidha, Lieber alituhumiwa kwa kuificha serikali ya Marekani, uhusiano wake na China na kudanganya juu ya suala hilo.

**NHK**

## WHO yaonya chanjo ya corona kuongezwa

**New York,** MAREKANI

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limeonya kuwa mataifa tajiri hayapaswi kutumia chanjo za nyongeza kama suluhisho la kudumu dhidi ya janga la virusi vya corona.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Tedros Ghebreyesus, alisema matumizi ya nyongeza ya chanjo huenda yakarefusha muda wa janga hilo la virusi vya corona badala ya kulimaliza kabisa.

Ghebreyesus pia alitahadharisha sherehe za mkesha wa Mwaka Mpya, zitakazofanywa kiholela bila ya kuzingatia masharti ya afya, zinaweza kuwa chanzo cha maambukizo mapya.

Hayo yanaarifiwa wakati Ufaransa ikiwa moja kati ya mataifa ya kwanza duniani kuanza kutoa chanjo kwa watoto wenye umri wa kati ya miaka mitano hadi 11, huku Uingereza ikiidhinisha chanjo ya Pfizer kwa watoto.

**DW**

# Tshisekedi awataka magavana kutatua migogoro kisiasa

**Kinshasa,** DRC

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Félix Tshisekedi amewataka magavana kwenye majimbo, kushirikiana na mabunge yao katika kukuza mshikamano wa kitaifa na umoja.

Tshisekedi ametoa rai hiyo wakati wa ufunguzi wa kikao cha nane cha kongamano la magavana linaloendelea jijini Kinshasa, huku akiwataka magavana wa mikoa yote 26 kutafuta suluhu ya migogoro ya kisiasa.

Pamoja na kukiri kudorora kwa uchumi, pia kukosekana kwa mipango mikakati ya kuboresha maisha ya raia kwenye majimbo, hali inayosababisha wabunge kwenye majimbo kutokuwa na imani kwa magavana hadi kuwafuta kazi.

Rais Tshisekedi alisema ni hali inayoeleweka na lazima kuwe na ushirikishwaji wa kila sekta, kwa ajili ya maendeleo ya jamii.

Kongamano hilo, limeandaliwa na idara ya kitaifa inayojihusisha na utawala wa majimbo katika Wizara ya Mambo ya Ndani, chini ya kauli mbiu 'Utulivu katika tawala za majimbo, hakikisho la mafanikio ya mpango wa maendeleo ya jamii'.

**RFI**




Wasafiri wakisubiri kukaguliwa kabla ya kuanza safari za msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka, wakiwa eneo la Hartsfield-Jackson, kwenye uwanja wa kimataifa Atlanta, Georgia, nchini Marekani, juzi. Licha ya kuwapo kwa maambukizi ya kirusi kipya cha omicron idadi ya wasafiri duniani imeongezeka. **PICHA: REUTERS**

# Wakimbizi wa DRC warejea Zambia

**Kinshasa,** DRC

OPERESHENI mpya ya kuwarejesha maelfu ya wakimbizi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kutoka Zambia, imeanza miongoni mwao wakiwa wamekaa nje ya nchi kwa miaka minne, kutokana na kuhofia maisha yao kufuatia mapigano.

Migogoro ya kikabila pamoja na mapigano kati ya majeshi ya usalama na makundi yenye silaha katika baadhi ya maeneo ya Kusini Mashariki mwa Congo, yalisababisha wimbi kubwa la wahamiaji kuelekea Zambia mwaka 2017.

Sasa hivi hali kwenye jimbo la Haut Katanga, ambako ghasia hizo zilishuhudiwa, inasemekana kuwa tulivu na hivyo kuruhusu kurejea kwa usalama kwa wakazi waliokimbia makwao.

Inasemekana kwamba karibu wakimbizi 5,000 wa DRC wamefanya uamuzi wa kurejea kwao kwa msaada wa Shirika la Kuhudumia Wakimbizi la Umoja wa Mataifa, (UNHCR), pamoja na serikali ya Zambia.

Kundi la kwanza la watu 100 limeondoka wiki hii kwenye eneo la Mantapala kwenye jimbo la Laupala nchini Zambia, likielekea kwenye kijiji cha Pweto, kilichoko kwenye jimbo la Haut Katanga, DRC.

Msemaji wa UNHCR, Babar Baloch, alisema kwamba hali ya usalama kwenye eneo hilo imeimarika kiasi cha kuruhusu wakimbizi kurejea kwao kwa njia salama na yenye heshima.

UNHCR, ilisema kwamba zoezi hilo litaendelea hadi mwaka ujao, hadi wote wanaotaka kurejea kwao watakapopata nafasi ya kufanya hivyo.

**VOA**

# SABABU KINACHOIKWAMISHA BIASHARA UNITED YAANIKWA

**Na Dennis Fussi**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Patrick Odhiambo, ameutupia lawama uongozi wa timu hiyo kwa kutotimiza majukumu yao kama inavyotakiwa na kusababisha kikosi chao kufanya vibaya katika mechi za Ligi Kuu, Tanzania Bara inayoendelea.

**Biashara United iliyomaliza nafasi ya nne msimu uliopita imekuwa na wakati mgumu msimu huu, katika michezo tisa iliyocheza imekusanya pointi nane huku ikishinda mchezo mmoja sare tano na kupoteza michezo mitatu.**

Odhiambo aliliambia gazeti hili binafsi hafurahishwi kuona timu yake ikipata matokeo mabaya katika kila mchezo, lakini viongozi wake wameshindwa kutimiza wajibu wao kwa kukamilisha vibali vya wachezaji wa kigeni waliosajiliwa.

"Tuna upungufu kwenye ushambuliaji na wachezaji wapo, lakini tunashindwa kuwatumia tatizo ni vibali na uongozi unalijua hilo lakini hawalifanyii kazi," alisema Odhiambo.

Kocha huyo alisema kwa namna mambo yanavyokwenda huenda atajiweka pembeni sababu matokeo mabaya yanamvurugia rekodi zake kitu ambacho siyo kizuri.

Aliongeza Biashara United ni timu nzuri na yenye wachezaji wenye vipaji, lakini inakosa washambuliaji ambao jukumu lao ni kumalizia mashambulizi yanayotengenezwa.

Kwa upande wake Ofisa Habari wa timu hiyo, Frank Wabare, alisema suala la wachezaji hao linakwamishwa na wizara husika, lakini wanapambana kuhakikisha wachezaji hao wanapata vibali, ili kuipigania timu hiyo.

Wabare alisema mchakato wa kumaliza changamoto hiyo sasa unaelekea mwishoni na wanaamini wataanza kupata matokeo mazuri kama ilivyokuwa msimu uliopita baada ya nyota hao kupata vibali.

Biashara United inatarajiwa kuwasili jijini Dar es Salaam leo, kwa ajili ya kuwakabili Yanga hapo keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.




Mwenyekiti wa kamati ya maandalizi ya mashindano ya kutafuta vitu vilivyofichwa, Dennis Rugemalila (kushoto), akizungumza kuhusu michezo hiyo itakayofanyika Desemba 30, mwaka huu, kwenye viwanja vya Kawe jijini Dar es Salaam. Kulia ni Mratibu, Godwin Lyimo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# *Kagera Sugar wamshangaza Baraza*

**Na Adam Fungamwangwo**

HAAMINI! Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza ameonyesha kushangazwa na wachezaji wake kutengeneza nafasi 19 za kufunga, lakini wameshindwa kupachika hata bao moja katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba dhidi ya Mbeya Kwanza.

Kagera Sugar ikiwa nyumbani ilikubali kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Mbeya Kwanza, yaliyowekwa wavuni na William Edgar na Oscar Mwansanga, licha ya kutawala karibuni dakika zote za mchezo.

"Tutakwenda kwenye uwanja wa mazoezi kuangalia namna ya umaliziaji kwa sababu imeonekana ni tatizo. Ni uchungu sana kuona tunatengeneza nafasi 19, lakini tunashindwa kufunga," alisema Baraza.

Mkenya huyo aliongeza timu yake ilitawala mechi nzima, lakini wapinzani wao Mbeya Kwanza walikuja na mkakati wa 'kupaki basi' na mfumo huo uliwasaidia kwa kiasi kikubwa kwa sababu pia walikuwa wakifanya mashambulizi ya kushtukiza.

Kocha Mkuu wa Mbeya Kwanza, Maka Mwalwisi, alisema waliingia na mfumo wa kukaa nyuma kutokana na kuiheshimu Kagera Sugar, ambayo ni moja ya timu nzuri katika Ligi Kuu Bara na yenye wachezaji bora.

Mwalwisi alisema mpango mkakati wao ni kucheza kwa nidhamu na kupata ushindi, ili kurudisha morali ya wachezaji ambao ilionekana imepotea.

## Kocha Mbeya City aifikiria Coastal

**Na Saada Akida**

WAKATI akijiandaa kukamilisha mapendekezo ya usajili wa dirisha dogo, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule amesema ameelekeza nguvu na akili zake katika michezo yake miwili inayofuata ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, imefahamika.

Mbeya City leo itakuwa ugenini Tanga dhidi ya Coastal Union na Desemba 27, mwaka huu itawafuata Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Ushirika Moshi, Kilimanjaro.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lule alisema mechi zote mbili ni ngumu kwa sababu watakuwa ugenini, lakini wamejipanga kupambana, ili kupata matokeo chanya.

Lule alisema baada ya mechi hizo mbili, watakaporejea nyumbani watakuwa na kikao maalumu cha kujadili nyota wapya anaowahitaji kwa lengo la kukiimarisha kikosi chake.

"Tunahitaji kupambana sio rahisi kupata matokeo katika michezo ya ugenini, hali ambayo nalazimika kuachana na suala la usajili na kutia nguvu katika hii mechi mbili na suala la usajili hii ni nafasi ya mwisho ya timu kuboresha, mwalimu unatakiwa kuwa makini na sio kukurupuka, hali hiyo tumalize hizi mechi mbili," alisema Lule.

## Tenesi wanaume, wanawake wajifua

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Tenesi Tanzania (TTA), kimesema tayari wameshapata vikosi vya timu za taifa za wanaume na wanawake, ambazo zitashiriki katika mashindano ya dunia ya mchezo huo yanayotarajiwa kufanyika mapema mwakani, imefahamika.

Mwenyekiti wa TTA, Dennis Makoi, alisema kwa sasa wanasubiri taarifa kutoka katika Shirikisho la Dunia la mchezo huo, ili kufahamu mahali ambapo michuano hiyo itafanyika.

"Tunashukuru kupata nafasi ya kwenda kushiriki mashindano ya dunia ya ambayo yatashirikisha mataifa mbalimbali, ili nafasi ya kujivunia kwetu, tumejipanga kwenda kupeperusha vyema bendera ya Tanzania," alisema Makoi.

Mwenyekiti huyo alisema mara baada ya kupata kupata tiketi ya kushiriki michuano hiyo, timu zao zilianza mazoezi kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam, ili kujiweka tayari na mashindano hayo.

"Tumeweka kambi hapa Dar es Salaam timu inanolewa na Kocha Mkuu, Salum Mvita, wakati kwa wachezaji waliopo mkoani Arusha wanafundishwa na Kocha, Godluck Molel, " Makoi alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TRIPPIER AGOMBEWA EPL

NEWCASTLE inakabiliwa na ushindani kutoka Manchester United na Tottenham Hotspur katika kinyang'anyiro cha kumwania mlinzi wa England, Kieran Trippier, 31, kutoka klabu ya Atletico Madrid. ***(90min)***

### JOHNSTONE AGEUKA LULU

TOTTENHAM, Newcastle, West Ham na Rangers wanagombania kumsajili mlinzi wa West Brom na Timu ya Taifa ya England, Sam Johnstone, 28. ***(Teamtalk)***

### AUBAMEYANG SOKONI

ARSENAL ipo tayari kusikiliza ofa kwa ajili ya mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, 32, baada ya kuvuliwa unahodha mwezi huu. ***(ESPN)***

### DIGNE ANUKIA NAPOLI

NAPOLI wanaangalia uwezekano wa kumpa mkataba beki wa Everton na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Lucas Digne, 28, ambaye amedokeza anataka kuondoka pale Goodison Park ifikapo Januari. ***(Foot Mercato)***

### UMTITI, COUTINHO WAGOMA

BARCELONA wanahangaika kumwachia mlinzi Mfaransa, Samuel Umtiti, 27, na mchezaji nyota wa Brazil, Philippe Coutinho (29), kwa sababu wachezaji wote wawili hawataki kuacha mikataba yao minono pale Nou Camp. ***(TodoFichajes)***

### SPURS, DELLE HAKIJAELEWEKA

TOTTENHAM Hotspur wanaangalia namna ya kuwaondoa kwende klabu hiyo mlinzi, Matt Doherty mwenye umri wa miaka 29 na kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Dele Alli (25). (The Athletic)

### DIAZ KUMRITHI MANE

LIVERPOOL wanawafuatilia kwa karibu winga wa Porto na Colombia, Luis Diaz, 24, kama mchezaji mbadala wa Sadio Mane (30), ambaye anaelekea kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa ajili ya kuitumikia Senegal itakayofanyika kuanzia mwezi ujao. ***(FourFourTwo)***

### DAVID NJIA MOJA

MSHAMBULIAJI wa Canada, Jonathan David, 21, ambaye anahusishwa na Arsenal na West Ham, ataondoka katika klabu yake ya Lille ya Ufaransa mwaka ujao, amesema wakala wake. ***(Radio Canada)***

### BAYERN YAMWANIA DEST

BARCELONA wako tayari kupokea ofa kwa ajili ya mlinzi wao raia wa Marekani, Sergino Dest, 21, huku Bayern Munich nao wakifuatilia hali yake. ***(ESPN)***

### KOLASINAC KUTUA WATFORD

WATFORD wana nia ya kumsajili mlinzi wa Arsenal, Sead Kolasinac, 28, ambaye ni raia wa Bosnia ifikapo Januari. ***(Telegraph)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SAHA AMTABIRIA MAKUBWA MBAPPE

**Asema Mfaransa huyo bado ana muda mrefu wa kuwa kwenye ubora wake...**

**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe ana uwezo wa kuendelea kufunga kwenye maisha yake ya soka na kucheza kwa muda mrefu sawa na Cristiano Ronaldo, bila kujali wapi atacheza msimu ujao.

**Hii ni kwa mujibu wa Louis Saha, ambaye pia anatarajia, Lionel Messi atang'ara sana kwenye Ligi Kuu Ufaransa maarufu Ligue 1, mara tu atakapokuwa fiti na kamili mwaka unaokuja.**

Mbappe yupo kwenye miezi yake sita katika mkataba wake na miamba hao wa Parc des Princes na yupo huru kusaini mkataba wa awali na klabu nyingine nje ya Ligue 1 kuanzia Januari.

Real Madrid ilituma ofa mbili ambazo zilikataliwa kwa ajili ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa katika madirisha yaliyopita na bado wanamwania nyota huyo kwa ajili ya mwaka 2022.

Mbappe amefunga mabao 15 na kutoa asisti 12 katika mechi 24 alizocheza kwenye mashindano yote msimu huu.

Na wakati Mbappe bado yupo kwenye Ligue 1 msimu wa 2021-22, Saha anaelewa Mfaransa mwenzake huyo anatarajia kufanya maamuzi makubwa kuhusu majaliwa yake wiki chache zijazo.

"Jambo kubwa kwangu mimi ilikuwa kwa yeye kubakia PSG mwaka huu," alisema Saha akinukuliwa na France Football.

"Chochote atachofanya kwa mwaka ujao, kwangu mimi ni sawa tu kwa sababu haya ni maisha yake ya soka.

"Tulitaka kuona Mbappe, Messi and Neymar wakicheza pamoja. Ni jambo la kuvutia kuona akiamua wapi anataka kwenda. Ni mchezaji ambaye anaweza kuamua mwenyewe kuhusu majaliwa yake."









# MENDY MAMBO YANAZIDI KUMWELEMEA

**MANCHESTER,** England

MCHEZAJI wa Manchester City, Benjamin Mendy, ameongezewa shtaka jingine katika mashtaka yake ya ubakaji.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, sasa anatuhumiwa kwa makosa saba ya ubakaji na shtaka moja la unyanyasaji wa kijinsia unaohusiana na wanawake watano.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 alishtakiwa wiki iliyopita kwa kosa la hivi sasa, lakini ilikuwa chini ya vikwazo vya kuripoti.

Vikwazo hivyo viliondolewa awali wakati Mendy alipowasili katika mahakama ya Chester Crown kwa ajili ya kusikilizwa kwa kesi yake.

Shtaka la hivi sasa linahusiana na mlalamishi mpya na linadaiwa kufanyika Julai, mwaka huu.

Makosa ya awali yanadaiwa kufanywa kati ya Oktoba, 2020 na Agosti, mwaka huu.

Mwanasoka huyo ambaye amekuwa kizuizini tangu kukamatwa kwake hapo Agosti, alionekana pamoja na mshtakiwa mwenzake, Louis Saha Matturie mwenye umri wa miaka 40, wa Eccles huko Greater Manchester.




# Chelsea vs Tottenhar
# Liverpool vs Arsenal

**LONDON,** England

CHELSEA itacheza na Tottenham Hotspur katika mechi ya nusu fainali ya Kombe la EFL, wakati Liverpool itaivaa Arsenal.

Chelsea ya Kocha, Thomas Tuchel iliichapa Brentford mabao 2-0 Jumatano kwa bao la kujifunga la Pontus Jansson na penalti ya Jorginho ndani ya dakika 10 za mwisho za mchezo huo.

Blues hao sasa watakutana na kocha wao wa zamani, Antonio Conte anayeinoa Tottenham ambayo ilishinda 2-1 dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja la London, West Ham.

Liverpool ilifuzu hatua hiyo baada ya kuifunga Leicester City kwa mikwaju ya penalti baada y wa kawaida kumalizika kwa


Baada ya sare hiyo kwa m kawaida, timu hizo ziliingia penalti na Liverpool ikashin

Na sasa vijogoo hao wa watavaana na Arsenal kwen fainali ya mashindano hayo

Washikabunduki hao v hatua hiyo baada ya kupa indi mtamu wa mabao 5-1 d Sunderland Jumanne, huku Eddie Nketiah akifunga 'hat-trick'.

Mechi za kwanza za nu ali hiyo zinapigwa wiki ya mwaka 2022, huku fainali y pangwa kucheza Februari kwenye dimba la Wembley.

## HABARI MICHEZO



# MOROCCO ALIA NA MABEKI NAMUNGO

**Na Dennis Fussi**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco, amesema wao wenyewe ndio 'waliutupa' ushindi katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Dodoma FC, juzi Jumatano.

Namungo ikicheza kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi walichezea kichapo cha mabao 2-1, huku wakipoteza nafasi nyingi za kufunga kipindi cha pili.

Akizungumzia mchezo huo, Morocco alisema timu yake ilicheza vibaya katika kipindi cha kwanza huku safu yake ya ulinzi ikishindwa kutimiza majukumu yake ipasavyo.

**Morocco alisema pia walishindwa kuzitumia nafasi nyingi walizozipata kipindi cha pili ambazo zingewasaidia kuondoka na pointi tatu.**

"Ninachoweza kusema mchezo wa leo (juzi) tumeutupa wenyewe, tulishindwa kabisa kutumia nafasi tulizozipata kipindi cha pili ili kufunga," alisema Morocco.

Aliongeza; "Pia safu yangu ya ulinzi ndio iliniangusha zaidi, kwa sababu ilishindwa kufanya kazi yake kwa utulivu na kwa umakini."

Hata hivyo, Morocco alisema sababu ya safu yake ya ulinzi kushindwa kufanya vizuri ni kutokana na kupanguliwa mara kwa mara, kwani hajawa kwenye upatina mzuri.

"Walinzi wangu hajawa na muunganiko kwa sababu kila tunapotengeneza 'upatina' na walinzi, mmoja au wawili wanaondoka na hivyo tunakuwa na kazi ya kuanza upya kutafuta tena muunganiko kila wakati," alisema.



Wachezaji wa timu ya soka la ufukweni ya Wakala Msomi wakifanya mazoezi kwenye Uwanja vya Karume Ilala jijini Dar es Saalam kwa ajili ya kujiandaa na mashindano mbalimbali watakayoshiriki hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Coastal Union yaendelea kujipanga*

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Coastal Union umesema hatima ya mshambuliaji wao mpya kutoka Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini Mzambia, Lewis Macha iko mikononi mwa Kocha Mkuu, Melis Medo .

Macha ana wiki mbili tangu ametua hapa nchini kwa lengo la kusajiliwa kipindi cha dirisha dogo kwa ajili ya kuimarisha kikosi cha timu hiyo ili kufikia malengo ya kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara .

Mwenyekiti wa Coastal Union, Steven Mnguto aliliambia gazeti hili jana tayari wamemkabidhi Medo uamuzi wa mchezaji gani anayemhitaji ili kuimarisha kikosi chake.

Mnguto alisema kuhusu Macha, aliyekuja hivi karibuni hajasajiliwa na badala yake kocha mkuu anahitaji kumwona zaidi kwa kufanya majaribio ili kufikia uamuzi.

"Huyo mchezaji ni kweli yuko nchini, suala la kumsajili liko mikononi mwa Kocha Mkuu ambaye amezuia uongozi kumsajili hadi hapo atakapofanya majaribio na kuridhishwa na kiwango chake," alisema Mnguto.

Aliongeza hawatarajii kufanya mabadiliko makubwa katika kikosi chao lakini akiweka wazi watabooresha safu ya ushambuliaji.


# 4,667,160

# JACKPOT
# MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/12/2021 | 18:00 | Peterborough vs Reading | 2.37 | 3.28 | 2.84 |
| 02. 26/12/2021 | 18:00 | Millwall vs Swansea | 2.29 | 3.19 | 3.04 |
| 03. 26/12/2021 | 18:00 | Hull City vs Blackburn | 2.90 | 3.19 | 2.37 |
| 04. 26/12/2021 | 18:00 | Preston vs Sheffield Utd | 2.90 | 3.25 | 2.34 |
| 05. 26/12/2021 | 18:00 | Portsmouth vs Oxford Utd | 2.43 | 3.28 | 2.75 |
| 06. 26/12/2021 | 18:00 | Lincoln vs MK Dons | 2.89 | 3.29 | 2.32 |
| 07. 26/12/2021 | 18:00 | Cheltenham vs Plymouth | 2.99 | 3.33 | 2.24 |
| 08. 26/12/2021 | 18:00 | AFC Wimbledon vs Charlton | 2.70 | 3.24 | 2.50 |
| 09. 26/12/2021 | 18:00 | Dundee Utd vs Hibernian | 2.90 | 3.15 | 2.42 |
| 10. 26/12/2021 | 18:00 | Kortrijk vs Royal Antwerp | 2.75 | 3.55 | 2.43 |
| 11. 26/12/2021 | 18:00 | Burnley vs Everton | 2.48 | 3.15 | 2.95 |
| 12. 26/12/2021 | 18:00 | Inverness vs Partick Thisle | 2.33 | 3.23 | 2.89 |
| 13. 26/12/2021 | 18:00 | Hamilton vs Kilmarnock | 2.72 | 3.26 | 2.43 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 24 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1144 | Prison Leopards vs Zesco United | 3.20 | 2.95 | 2.43 |
| 14:00 | 2078 | Girona FC B vs Peralada CF | 2.18 | 2.80 | 3.52 |
| 14:30 | 1592 | MES Rafsanjan vs Nassaji Mazandaran | 1.82 | 3.08 | 4.43 |
| 14:30 | 2538 | Aluminium Arak vs Gol Gohar | 2.00 | 2.84 | 4.05 |
| 14:30 | 3550 | Padideh Mashhad vs Esteghlal Tehran | 8.48 | 4.15 | 1.35 |
| 14:30 | 4165 | Havadar vs Teraktor Sazi | 2.44 | 2.78 | 3.02 |
| 14:30 | 5471 | Naft Masjed Soleyman FC vs Fajr Sepasi | 2.56 | 2.75 | 2.90 |
| 15:00 | 2413 | Adama City FC vs Bahir Dar Kenema FC | 4.53 | 3.23 | 1.75 |
| 15:45 | 2378 | Masafi vs Masfoot Sports Club | 2.66 | 3.87 | 2.15 |
| 15:45 | 3228 | AL Jazira AL Hamra vs Ahli Al-Fujirah | 4.32 | 4.03 | 1.61 |
| 16:00 | 1736 | Hapoel Afula vs Ahi Nazareth | 2.73 | 2.97 | 2.73 |
| 16:00 | 2031 | Maccabi Bney Reine vs Hapoel Ramat Gan | 1.69 | 3.43 | 5.37 |
| 16:00 | 2395 | Bnei Yehuda vs Hapoel Petah Tikva | 2.06 | 3.13 | 3.78 |
| 16:00 | 2728 | Ceramica Cleopatra vs Arab Contractors | 2.16 | 3.15 | 3.40 |
| 16:00 | 3316 | KMC vs Simba | 5.19 | 3.17 | 1.69 |
| 16:00 | 3570 | AS Ashdod vs Ironi Hasharon | 2.13 | 3.13 | 3.57 |
| 16:00 | 4069 | Hapoel Kfar Saba vs Hapoel Acre | 2.01 | 3.31 | 3.71 |
| 16:00 | 4229 | Hapoel Raanana vs El Fahem | 2.68 | 3.03 | 2.73 |
| 16:00 | 4253 | Coastal Union vs Mbeya City | 2.85 | 2.51 | 2.85 |
| 16:00 | 4410 | Hapoel Rishon Lezion vs Beitar Tel Aviv Ramla | 1.86 | 3.42 | 4.16 |
| 16:00 | 5368 | Sectzya Nes Ziona vs SC Kfar Qasem | 2.57 | 3.07 | 2.82 |
| 16:00 | 5786 | Kabwe Warriors vs Zanaco | 2.04 | 2.93 | 3.74 |
| 16:05 | 1679 | Al Ahli Doha SC vs Al-Sailiya SC | 2.37 | 3.26 | 2.69 |
| 16:05 | 3808 | AL Wakrah vs Al-Shamal | 1.52 | 4.03 | 5.18 |
| 16:05 | 5219 | AL Nasr vs AL Arabi | 3.14 | 3.57 | 2.00 |
| 16:30 | 1097 | Sepahan Esfahan vs Peykan FC | 1.51 | 3.56 | 6.35 |
| 16:30 | 1932 | Altinordu vs Boluspor | 3.04 | 3.24 | 2.16 |
| 16:30 | 5363 | Foolad Khuzestan vs Sanat Naft Abadan | 1.66 | 3.14 | 5.60 |
| 16:30 | 5956 | Persepolis FC vs Zob Ahan | 1.46 | 3.76 | 6.76 |
| 17:00 | 1997 | Ol. Medea vs Paradou AC | 2.21 | 3.19 | 3.00 |
| 17:00 | 3198 | HB Chelghoum Laid vs ASO Chlef | 2.37 | 3.18 | 2.75 |
| 17:00 | 4525 | RC Arbaa vs WA Tlemcen | 2.17 | 3.13 | 3.13 |
| 17:00 | 4688 | NA Hussein Dey vs MC Alger | 2.59 | 3.12 | 2.54 |
| 17:00 | 4928 | US Biskra vs CR Belouizdad | 2.89 | 3.18 | 2.27 |
| 17:00 | 5533 | Delhi Dynamos FC vs FC Goa | 2.74 | 3.37 | 2.28 |
| 18:00 | 1096 | ES Setif vs CS Constantine | 2.01 | 3.18 | 3.47 |
| 18:00 | 2196 | Wydad Casablanca vs Mouloudia Oujda | 1.44 | 3.94 | 6.54 |
| 18:00 | 4502 | Bassam vs LYS Sassandra | 4.44 | 2.85 | 1.91 |
| 18:00 | 4620 | Hawassa Kenema SC vs Arba Minch Kenema | 2.60 | 2.79 | 2.79 |
| 18:15 | 5617 | Qatar SC vs Al Rayyan SC | 3.94 | 3.65 | 1.75 |
| 18:30 | 4618 | Eastern Company SC vs Farco FC | 7.09 | 4.04 | 1.46 |
| 18:45 | 2084 | Yarmouk vs Al Shabab Kuwait | 4.30 | 4.00 | 1.73 |
| 19:00 | 3812 | JS Saoura vs MC Magra | 1.56 | 3.67 | 5.41 |
| 19:00 | 4944 | Adanaspor vs Kocaelispor | 2.41 | 3.18 | 2.70 |
| 19:00 | 5324 | JS Kabylie vs RC Relizane | 1.62 | 3.36 | 5.38 |
| 20:00 | 3587 | USM Alger vs MC Oran | 1.64 | 3.46 | 5.00 |
| 20:15 | 5813 | Sccm Chabab Mohammedia vs RS Berkane | 2.36 | 2.89 | 3.03 |
| 21:00 | 2221 | Al Masry Club vs El Ittihad Alexandria | 2.28 | 2.96 | 3.35 |
| 21:00 | 4572 | ASEC Mimosas vs Asi D Abengourou | 1.27 | 4.35 | 12.56 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


m,
a muda
3-3.
nuda wa
kwenye
da 5-4.
Anfield
ye nusu
valifuzu
ta ush-
dhidi ya
u kinda
matatu
su fain-
pili ya
yake iki-
27 pale

# Michezo

Ijumaa Desemba 24, 2021

Nipashe





Chelsea vs Spurs, Liver vs Arsenal

UKURASA 22

MAUAJI...



Wachezaji wa Simba Queens wakishangilia moja ya bao lililofungwa katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (SWPL), iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mo Arena Bunju, Dar es Salaam. Simba Queens ilishinda mabao 15-0. **PICHA: SIMBA SC**

## Mrithi wa Diarra aivuruga Yanga

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikipangwa kuanza kampeni ya kuwania ubingwa wa Kombe la Mapinduzi Zanzibar kwa kuvaana na Taifa Jang'ombe Januari 5, mwakani, uongozi wa timu hiyo uko katika mipango ya kunasa saini ya golikipa mzawa ili kurithi mikoba ya Djigui Diarra atakayekwenda kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2022), nchini Cameroon akiwa na kikosi cha Mali.

Mohammed Makaka wa Ruvu Shooting, Abdultwalib Mshery (Mtibwa Sugar) na Haroun Mandanda wa Mbeya City wanatajwa kutua katika klabu hiyo ambayo tayari imeshatangaza kuachana na Ramadhani Kabwili.

Taarifa kutoka katika klabu hiyo zinasema Yanga inahitaji kuimarisha eneo hilo kwa sababu baada ya Diarra kuelekea AFCON, timu itabakia na kipa mmoja tu, ambaye ni Erick Johora.

"Diarra hana wa kumpa ushindani, tumeingia sokoni kusaka mtu ambaye atakuwa bora langoni hata asipokuwapo, akiwa katika majukumu ya kuiwakilisha nchi yake, hatutakuwa na presha kuhusu mbadala wake," kilisema chanzo chetu.

Chanzo hicho kilisema nafasi ambayo 'inawaumiza kichwa' na wanahitaji kuiimarisha zaidi katika kipindi cha dirisha dogo la usajili ni ya golikipa.

"Suala la usajili limeshafika kwa uongozi na nina imani kila kitu kitaenda vizuri, kazi yangu kubwa kwa sasa ni kuhakikisha tunaendelea kuimarika na kutafuta pointi muhimu katika michezo hiyo iliyopo mbele yetu," Nasreddine Nabi, Kocha Mkuu wa Yanga alisema.

Aliyekuwa kiungo wa Azam FC, Salum Aboubakar 'Sure Boy' na winga wa Biashara United, Dennis Nkane wameshakamilika usajili wa kujiunga na Yanga.

Wakati huo huo, katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi, Yanga imepangwa katika Kundi B ikiwa na Taifa Jang'ombe na KMKM huku Simba ikiwa Kundi C pamoja na Selem View na Mlandege wakati Kundi A linaundwa na Azam FC, Namungo, Yosso Boys na Meli 4 City.

# Simba, KMC FC hapatoshi Bara

## Mabingwa watetezi waahidi kuwapa heshima mashabiki wao huku...

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

BAADA ya wiki iliyopita kukutwa na changamoto ya wachezaji wake kuugua homa, mafua na kukohoa, mabingwa watetezi, Simba wanatarajia kuwavaa wenyeji KMC FC katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora.

**Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa Simba Mhispania, Pablo Franco, alisema mechi hiyo inatarajiwa kuwa ngumu kwa sababu wachezaji wake wametoka kwenye changamoto ya kiafya, huku nyota wake wengine bado afya zao hazikuimarika.**

Pablo alisema licha ya hali hiyo, wamejiandaa kupambana kuhakikisha wanapata ushindi na kuendelea kuwakimbiza vinara wa ligi hiyo, watani zao, Yanga.

"Hatukucheza mechi iliyopita, unajua afya ni muhimu kwanza, lakini tumekuja kucheza mechi hii tukiwa tumeimarika, itakuwa mechi ngumu, tumejiandaa kufanya vizuri kadri tutakavyoweza ili kuhakikisha tunapata ushindi, tutaangalia mpaka mchana, wachezaji ambao watakuwa wako vizuri kwa ajili ya mechi ndio tutawatumia," alisema Pablo.

Meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu, alisema kikosi chao kiko vizuri na wamejiandaa kukutana na ushindani kutoka kwa wapinzani.

Rweyemamu alisema walisafiri na kikosi cha wachezaji 24, ambao wako tayari kwa mchezo huo ambao unazikutanisha timu zinazofahamiana vyema.

"Wachezaji wetu wapo vizuri na tayari kuwakabili KMC, tunajua mchezo huu ni muhimu kama ilivyo michezo mingine, ingawa tulishindwa kucheza mchezo uliopita kutokana na kupata changamoto ya kiafya, tutapambana kwa ajili ya kupata pointi tatu za ugenini," alisema Rweyemamu.

Meneja huyo aliongeza wanajua mechi zote za ligi ni ngumu na hasa katika mzunguko huu wa kwanza ambao kila timu inahitaji kujiweka kwenye nafasi nzuri ili kutimiza malengo.

"Kila timu ina malengo yake, kabla ya kuanza msimu tunaweka mikakati ambayo 'tunaishi' nayo msimu mzima, hivyo hautakuwa mchezo mwepesi, na tunajua tunacheza kwenye uwanja wa aina gani," Rweyemamu alisema.

Aliongeza wachezaji waliokuwa wagonjwa wanaendelea vyema na wanashukuru kwa mapokezi makubwa waliyopewa na mashabiki wa Tabora na kuahidi hawatawaangusha.

"Tunawashukuru mashabiki wetu wa Tabora kwa kutuonyesha ushirikiano mkubwa jana (juzi), tulipofika, na sisi hatuwezi kuwaangusha, tutapambana ili kuhakikisha tunaondoka na pointi zote muhimu," Rweyemamu alisema.

Naye Kocha wa KMC, Habib Kondo, alisema wataingia kucheza mechi hiyo kwa mfumo maalumu ambao wameufanyia mazoezi ili kuidhibiti Simba na endapo wachezaji wake watatekeleza vyema maelekezo, basi ana uhakika watapata pointi tatu.

"Sisi matayarisho yetu yaliisha tangu Dar es Salaam, tunacheza na mabingwa wa nchi, timu ya watu wengi na timu bora, lakini mara nyingi sisi tukicheza na timu bora, nasi tunakuwa bora, kila timu itakuja na 'plan' yake. Sisi wenyewe tumekuja na 'plan' yetu ambayo tutaitumia kwenye mechi hii, licha ya baadhi ya wachezaji kutokuwa vizuri, tunawaahidi mashabiki wetu ushindi," alisema Kondo.

Rekodi zinaonyesha KMC haijawahi hata kutoa sare au kushinda kwenye mechi yoyote ile ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba tangu ilipopanda daraja msimu wa 2018/19.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 9

9 770856 541002 >